**CHADEMA** yampa Samia mambo manane

UKURASA 3



**Wahusika** kifo cha mtangazaji ITV wasakwa

UKURASA 4


# Nipashe

Jumanne Machi 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580535

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**Defoe amwambia Kane aondoke Spurs**

UKURASA 21

MAKAMU WA RAIS

# Moshi mweupe wasubiriwa

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MKALIMANI MAZISHI YA JPM AFUNGUKA**

MKALIMANI Matungwa Mutatina, aliyekuwa akitafsiri hotuba...

UKURASA WA 7

**SEKTA YA MADINI YAINGIZA BIL. 400/- MIEZI MINANE**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema ndani ya miezi minane...


## ...Rais apewa sifa kila sehemu

UKURASA 3





Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MTANDAO**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store




# Asasi za kiraia zaomba kukutana na Samia

UKURASA 2


**MICHEZO** **YANGA YAFUNGUKA MUKOKO KAIZER CHIEFS** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Moshi mweupe wasubiriwa

**Na Salome Kitomari**

MACHO na masikio ya Watanzania yako jijini Dodoma kusubiri kuonekana kwa moshi mweupe katika jengo la Bunge litakalokuwa na wajibu wa kikatiba kupigia kura jina la Makamu wa Rais, litakapowasilishwa kwenye jengo hilo.

Vikao vya Bunge la 12 vinaanza leo ikiwa ni mkutano wa tatu tangu kuanza kazi kwa kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Tano Novemba 5, mwaka 2020, baada ya kushinda uchaguzi na kutangazwa rasmi Oktoba 28, mwaka huu.

Baadhi ya majina ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), yanatajwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kushika nafasi hiyo, lakini kitendawili hicho kinatarajiwa kuteguliwa wakati wowote bungeni.

Nafasi ya Makamu wa Rais ipo wazi tangu Machi 19, mwaka huu, baada ya aliyekuwa kwenye nafasi hiyo, Samia Suluhu Hassan, kula kiapo cha kuwa Rais wa Tanzania, kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Ili kumpata makamu wa rais kwa mujibu wa Katiba ni lazima rais apeleke jina pendekezwa kwenye chama chake na baadaye kupigiwa kura na Bunge.

Ibara ya 37 (5) inaeleza kuwa endapo kiti cha rais kitakuwa wazi kutokana na rais kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi ya mwili au kushindwa kutekeleza kazi na shughuli za rais, basi Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano.

Rais Hayati Dk. John Magufuli alifariki Machi 17, mwaka huu, na kiti cha rais kilibaki wazi na kujazwa na makamu wake kikatiba.

Katiba inasema kwa masharti katika ibara ya 40, kisha baada ya kushauriana na chama cha siasa anachotoka, Rais atapendekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura zisizopungua asilimia hamsini ya wabunge wote.

Ibara ya 40 (4) inasema endapo Makamu wa Rais anashika kiti cha Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 37(5) kwa kipindi kinachopungua miaka mitatu, ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara mbili, lakini kama akishika kiti cha Rais kwa muda wa miaka mitatu au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara moja pekee.

Kutokana na msingi uliowekwa na Katiba, Watanzania wanasubiri kwa hamu jina litakalopelekwa kwenye Kamati Kuu ya CCM ambayo baada ya kuridhika nalo litapelekwa bungeni.

Baadhi ya wanaotajwa katika nafasi hiyo ni wanasiasa vijana wenye ushawishi ambao kwa kiasi kikubwa wamekitumikia chama hicho kwa muda mrefu na ambaye ni msomi mwenye uelewa wa masuala ya uongozi na utawala.

Aidha, kingine ni mwenye diplomasia ambaye ataendeleza na kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine duniani, uzoefu wa siasa za Tanzania na nje, mwenye ushawishi na asiyeweza kumfunika rais wake katika utekelezaji wa majukumu yake.

Ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa na Makamu wa Rais mwanamke, ambaye sasa amekuwa Rais na kigezo cha uwiano wa rais mwanamke na makamu mwanaume kinaweza kuwa na nguvu dhidi ya kile cha kuwa na rais mwanamke na makamu wake mwanamke.

Ingawa wachambuzi wa masuala ya siasa wanasema awamu zilizopita ziliongozwa na wanaume, yaani Rais na Makamu wake, lakini kutokana na ugeni kwa jinsia hiyo (mwanamke) itakuwa ngumu kuwa na wanawake wote hasa ikizingatiwa aliyekuwa rais ni mwanaume.

Akitoa maoni yake, Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba, Bob Wangwe, alisema Makamu wa Rais anatakiwa awe mtu ambaye hawezi kutofautiana na mwelekeo wa Rais Samia lazima ashabihiane naye.

"Makamu hatakiwi awe ni Makamu wa Rais mwenye vinasaba vya kukandamiza demokrasia, asasi za kiraia na ambaye hataona haya kuitamka haki na kuisimamia. Kama ataweza kasi yake atamsaidia sana kwa kuwa Rais Samia ni mwenye busara, anasikiliza na anajali demokrasia," alisema.

Naye Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema matarajio ya Watanzania ni kuwa Rais atachagua mtu atakayeendana na viwango na kasi yake ya uongozi ambayo imeonekana kuwa ni mfuatiliaji na anachukua hatua kwa kuzingatia utawala wa sheria.

"Tunatarajia chama chake watamsikiliza na kushirikiana naye kupata mtu ambaye ni msaada kwake, kwa sasa tunaona Makamu wa Rais ni muhimu sana maana Rais asipokuwapo anachukua madaraka."

"Asipitishwe mtu kwa ushabiki bali kwa maslahi mapana ya nchi, wasiangalie kundi fulani bali awe mtu yeyote ambaye muda wowote anaweza kuwa rais, hivyo waangalie kwa mapana yake, kama tungekosea kuchagua Makamu wa Rais leo yangezungumzwa mengine."

# Asasi zaomba kukutana na Samia

**Na Beatrice Shayo**

ASASI za kiraia zaidi ya 200 nchini zimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan huku wakiomba kupatiwa fursa ya kukutana naye ili kupata dira ya mahitaji yake ya namna bora ya kuendeleza na kuimarisha ushirikiano kati yao na serikali.

Tamko hilo limetolewa jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari wakitoa salamu za pole kwa kifo cha aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli na pongezi kwa Rais Samia.

Akisoma kwa niaba ya tamko hilo Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema matumaini yao kadri ratiba yake itaruhusu wanaomba wakutane naye ili waweze kujadiliana mambo mbalimbali ya asasi za kirai.

"Matumaini yetu kuwa kadri ambavyo ratiba yake itaruhusu Rais Samia atatupa fursa ya sisi kama wadau wa asasi za kiraia kukutana naye ili kupata dira na mahitaji yake ya namna bora ya kuendeleza na kuimarisha ushirikiano kati ya asasi za kiraia na idara mbalimbali za serikali," alisema Olengurumwa.

Aidha, alisema wana imani atakwenda kufanya maboresho katika mfumo wa utoaji wa haki kwa wananchi kwa kuwa ni eneo ambalo wamelipigie kelele kwa muda mrefu.

Alisema kwa kitendo cha Rais Samia kuagiza kesi zisizo za msingi zifutwe gerezani ni jambo nzuri, ili kuwepo na upatikanaji wa haki.

"Tunampongeza Rais wetu tunaimini kabisa yale aliyoyasema juzi ni vitu ambavyo vipo moyoni mwake na ataendelea kuvipigania lakini sisi asasi za kiraia huo umekuwa ni wimbo wetu tuwe na mfumo mzuri wa utoaji wa haki."

"Kusiwe na watu wengi wanakaa mahabusu haki za watu ziheshimiwe ndio maana tunasema tunampongeza na tuna imani kuwa yale mambo ambayo tumekuwa tukiomba yafanyiwe kazi yamepata mtu ambaye anakwenda kuyaboresha zaidi hasa kwenye mfumo wa kisheria hapa nchini."

Aidha, alisema asasi hizo zinatarajia kuendelea kuboresha na kufanya kazi kwa karibu zaidi na serikali ili kuhakikisha wanachangia katika mafanikio ya Rais Samia.

"Tutaendelea kuboresha utendaji kazi wa asasi za kiraia na hivyo kuongeza tija katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa mfano sisi wadau wa asasi za kiraia tutaendelea kusaidia kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu za afya, elimu na maji.



Alisema pia watachangia ongezeko la utawala bora katika taasisi za kiserikali kutokana na ufuatiliaji utakaoendelea kufanywa na asasi za kiraia na haki za wadau mbalimbali wa utawala bora na haki za binadamu.

"Tutashirikiana na serikali kutoa huduma za kijamii kwenye maeneo mbalimbali na kuweka mikakati na serikali ya namna ya kutoa ajira kwa maelfu ya vijana Tanzania," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba, Bob Wangwe, alisema ni imani yake kuwa kutokana na kazi kubwa alizozifanya Rais Samia katika nafasi mbalimbali alizoshika ataendelea kutumia uzoefu wake kuhakikisha taifa linaendelea kupata maendeleo hasa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mkurugenzi wa mradi wa ushiriki wa wanaume katika kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Tiba), Marcela Lungu, alisema wanatoa salamu za pole kwa Rais Samia kutoka na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Anasema wana imani na Rais Samia kwa utendaji kazi uliotukuka katika kipindi chote cha uongozi wake kwenye nafasi mbalimbali alizowahi kushika kipindi cha nyuma.

## Mkalimani mazishi ya JPM afunguka

**Na Christina Mwakangale**

MKALIMANI Matungwa Mutatina, aliyekuwa akitafsiri hotuba za wageni wa kimataifa wakiwamo marais waliohudhuria mazishi ya kitaifa ya Hayati Dk. John Magufuli, jijini Dodoma, ameeleza sababu ya kutafsiri tofauti hotuba ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa.

Akihojiwa na kituo kimoja cha radio, jijini Dar es Salaam, alisema sababu ya kutokea kwa tatizo hilo ni uhaba wa vifaa vya kusikilizia na kusababisha kutoyasikia vizuri maneno ya mzungumzaji. Pia alisema mazingira yasiyo rafiki kufanya kazi yake ipasavyo yalimsababishia kutoyasikia maneno vizuri na aliamua kuwaomba radhi Watanzania alipogundua tafsiri yake haikuwa sahihi.

Muda mfupi baada ya tukio hilo kutokea, mkalimani huyo ambaye alikuwa akitafsiri hotuba ya Rais wa Afrika Kusini, alipata umaarufu wa ghafla mitandao ya kijamii baada ya kugundulika kutafsiri tofauti ya hotuba iliyotolewa.

Akizungumza na kituo hicho cha redio, Mutatina alisema baada ya kuona kumeibuka kicheko kutoka kwenye hadhira kulimfanya abaini amekosea.

"Sikusikia vizuri kilichotamkwa na mzungumzaji, pia baada ya kuona watu wamecheka. Niligundua kuna tatizo limetokea," alisema.

"Kile kicheko cha watu kilinifanya nijue nimekosea ikanibidi nibadili kutafsiri kinyume, kwenda mbele kwa kurudi nyuma. Baada ya kusikia kwa usahihi ndipo nikatoa tafsiri sahihi."

Pia alifafanua kuwa yeye ni mzungumzaji wa lugha tatu kubwa za kimataifa kwa ufasaha, kikiwamo Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa pamoja na lugha za makabila ambazo ni Kisukuma, Kinyambo na Kihaya.

Alisema ukalimani upo wa aina tatu ikiwamo wa papo kwa papo ambao hutumia vifaa maalum huku mzungumzaji akionekana na katika hadhira, huku mkalimani akiwa kwenye vizimba bila kuonekana akipokea sauti pekee ya mzungumzaji.

Mkalimani anakuwa haonekani na watu katika vizimba anapotafsiri, yaani tofauti inaweza mkapishana kwa sekunde chache, hata hadhira ikicheka isipishane muda sana na ulichoongea," alisema Mutatina.

"Rais Ramaphosa alisema: I felt honored because President Magufuli was not a great traveler, he didn't like to travel very much, he preferred to stay here at home...nilitafsiri hivi: Nilijisikia kuheshimiwa sana kwa sababu mheshimiwa Magufuli alikuwa mtu imara mwenye upendo ambaye alipenda kusikiliza na kutoa mwongozo kwa wenzake."

Nilipoona niko tofauti, nikaamua kutafsiri kwa kurudi nyuma, nikarudia tafsiri: Ninakumbuka mheshimiwa Magufuli alipendelea sana kukaa nyumbani kuliko kutembelea nchi za nje kwa sababu ya watu wake wa Tanzania...kumradhi kwa kutosikia vizuri," alisema Mutatina.

HABARI KITAIFA

## ...CHADEMA yampa mambo manane

**Na Mauld Mmbaga**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimempa Rais Samia Suluhu Hassan, mambo manane ambayo yanapaswa kuzingatiwa kupata Makamu wa Rais kwa mujibu wa katiba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, sekretarieti ya chama hicho imeona kuna haja ya wao kama chama kutoa maoni na mapendekezo yao kwa ajili ya kushauri na kuondokana na mgogoro wa kikatiba unaoweza kujitokeza.

La kwanza, baada ya Rais Samia kushauriana na chama chake atatakiwa kupendekeza na kuteuwa jina la mtu atakayekuwa makamu wake na mtu huyo atatakiwa kuthibitishwa na Bunge.

La pili, kwa kuwa Rais alishaapishwa na kushika madaraka kama ilivyoelezwa kwa mujibu wa Katiba, anatakiwa kuteuwa jina la Waziri Mkuu mapema ndani ya siku 14 tangu alipokula kiapo cha kushika madaraka ya urais.

La tatu, Rais anatakiwa kuteua jina la Waziri Mkuu na aliyekuwa Waziri Mkuu anakoma kuwa na nafasi hiyo isipokuwa kama atateuliwa tena na kula kiapo mbele ya Rais Samia.

La nne, kwa mujibu wa Katiba mawaziri na makatibu wao hawataanza kazi mpaka wale kiapo mbele ya Rais Samia, kwa sababu Rais anatakiwa kumteua Waziri Mkuu mwingine na atakula kiapo mbele yake baada ya kuthibitishwa na Bunge, hivyo baraza lote la mawaziri lililokuwapo kabla ya Rais kuapishwa linakoma kwa sababu ya kiti cha Waziri Mkuu kuwa wazi.

La tano, nafasi ya Waziri Mkuu au mawaziri na manaibu ni nafasi za uteuzi kulingana na uteuzi na ridhaa ya Rais, wanatakiwa kula kiapo mbele yake na kwa maana hiyo nafasi hizo si za kudumu kama ambazo hoja zinajengwa na baadhi ya wadau.

La sita, Ibara ya 37(10) inamtaka Rais aliyeshika madaraka kwa mujibu wa ibara ya 37 hatakuwa na mamlaka ya kuvunja bunge kuondoa uteuzi wa waziri au kufuta uteuzi wowote uliokuwa umefanywa na Rais.

La saba, "kila Rais mteule na kila mtu atakayeshikilia kiti cha Rais kabla ya kushika madaraka ya Rais ataapa mbele ya Jaji Mkuu wa kiapo cha uaminifu na kingine chochote kinachohusika na uteuzi wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na bunge."

La nane, Waziri Mkuu wa sasa na mawaziri wake waliapa kiapo cha utii mbele ya Hayati Rais John Magufuli na siyo kwa aliyekuwa makamu wake, na kwa maana hiyo ndiyo maana Rais wa sasa alipokuwa makamu alikula kiapo tofauti na sasa.

Alisema Rais Samia anao wajibu wa kuteuwa Waziri Mkuu mwingine kwa mujibu wa Katiba na kwa kushauriana na Waziri Mkuu atakayemteua afanye uteuzi wa mawaziri na manaibu wao ambao watatakiwa kula kiapo mbele yake.

"Ni maoni yetu kwamba Rais Samia atasimamia utaratibu uliopo kikatiba ili kuliepusha taifa na mgogoro wa kikatiba unaoweza kulikumba taifa letu," alisema Mnyika.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akijibu hoja za wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo walipokutana jana, Bungeni jijini Dodoma kwenye kikao cha kamati hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadau wammiminia Rais Samia sifa kila kona

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Rais Samia Suhulu Hassan, kupokea ripoti kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG), pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wachambuzi wameipongeza kasi aliyoanza nayo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, walisema hatua aliyoanza Rais Samia ikiwamo kuchukua hatua, kutoa maagizo na inaonyesha mwanzo mwema na wa aina yake.

"Rais Samia ameanza vizuri sana, pamoja na kwamba amekuwa katika pilika pilika za kutoka kumhifadhi katika nyumba yake ya milele mtangulizi wake, kama binadamu lazima alikuwa amechoka.

"Hakuacha kupiga kazi, amepelekewa ripoti kama alivyosema na kuipitia usiku kwa usiku na kuchukua hatua za haraka," alisema Dk. George Kahangwa, Mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alisema ni jambo jema na litasaidia wasaidizi wake pamoja na watumishi wa umma kufanya kazi kwa uaminifu na uzalendo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema rais ameonyesha mwanzo mzuri, alipochukua hatua na kuzingatia misingi ya sheria na haki za binadamu.

"Kama ambavyo rais alivyoanza kwa kuchukua hatua kwa kuzingatia misingi ya sheria.

"Kwa mfano Mkurugenzi wa TPA, amemsimamisha kwa kusema kwamba anapisha uchunguzi na hivyo ndivyo sheria inavyotaka," alisema Henga.

"Hata alipotoa maagizo mengine kwa wote aliona wanafanya uzembe, tulisikia anatoa maelekezo kwa mamlaka husika za uchunguzi, kwa hiyo katika suala la kusimamia haki za binadamu na utawala bora sisi kama LHRC, tumeweka vema kwa Rais wetu Samia."

**KUHUSU ATCL**

Dk. Kahangwa alisema kuna haja ya kufanya uchunguzi zaidi na kuweka wazi mambo ambayo yamesababisha shirika hilo kujiendesha kwa hasara.

"Watanzania tunayo haki ya kujua ni mambo gani ya msingi yamesababisha tumefikia katika hatua hiyo, kwa hiyo uchunguzi ufanyike zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa ripoti ya CAG, ATCL imekuwa ikijiendesha kwa hasara miaka mitano mfululizo na mwaka huu wa fedha ilijiendesha kwa hasara ya Sh. bilioni 60.

**HALMASHAURI DHAIFU**

Aidha, kuhusu halmashauri ambazo hazifanyi vizuri, walisema kuna haja ya serikali kuimarisha uwajibikaji katika eneo hilo kwa sababu halmashauri nyingi zimekuwa zikirudia makosa yaleyale ya kila mwaka.

"Kuna haja ya kuimarisha uwajibikaji kwenye halmashauri zetu, unapoona shida inaendelea tena na tena ina maana hapo kuna watendaji ambao hawatoshi katika nafasi zao au ni wavivu," alisema Dk. Kahangwa.

**THDRC**

Mratibu wa Mtandao wa Haki za Binadamu (THDRC), Onesmo Ole Ngurumo, alimpongeza Rais Samia kwa mwanzo aliouonyesha katika ripoti CAG.

Kadhalika, aliipongeza ripoti wa CAG kwa kitendo cha kuwa wawazi na kuliomba bunge likafanyie kazi taarifa hiyo ili kulijenga taifa.

"CAG kuandaa ripoti nzuri ni jambo jingine sasa ripoti yake kwenda kutekelezwa ni jambo jingine hata CAG Prof. Mussa Assad, alikuwa akilalamikia kazi yao ni kuandaa ripoti ingawa wanaokwenda kutekeleza ni watu wengine.

"Rais Samia ameonyesha ubora mkubwa na mwanzo mzuri kwamba ripoti za wataalamu zinavyotengenezwa inatakiwa iwe ya uwazi na ukweli na wanaotakiwa kutekeleza watekeleze bila kusitasita," alisema Ngurumo.

"Hizi ndio silaha ambazo rais anaweza kuzitumia. Silaha ambazo anaweza kuzitumia cha kuanza ni vyombo vya habari ambavyo vinaweza kutumika na kuibua mambo mengi ya rushwa.

**WACHUMI**

Mtaalamu wa masuala ya uchumi, Prof. Godius Kahyarara, aliishauri serikali kuongeza umakini katika kutoa ajira za utumishi na uteuzi, hasa nafasi za watendaji ili kudhibiti ubadhirifu kwenye mashirika ya umma.

Alisema ili kudhibiti vitendo vya ubadhirifu kwenye taasisi za umma ikiwamo halmashauri ni vyema kuhakikisha wanaoajiriwa ama kuteuliwa kwenye nafasi hiyo ni waadilifu.

"Hatua alizochukua Rais Samia nimepokea 'in positive way' (mtazamo chanya) ni mwendelezo wa utamadni wa serikali katika kuchukua hatua, umekuwa ukichukulia na serikali karibu zote, unaweza kukumbuka hata ilivyokuwa kwa Richmond," alisema Prof. Kahyarara.

**VIONGOZI WA DINI**

Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, Dk. Owdenburg Mdegela, alisema kasi aliyoanza nayo Rais Samia ya kutumbua wazembe ni nzuri na haina tofauti na ile ya mtangulizi wake, Hayati Dk. Magufuli.

"Pia hili suala la kesi kutosikilizwa kwa wakati tayari lilikwisha zungumzwa na Magufuli kwa kutaka mrundikano wa kesi ushughulikiwe haraka."

***Imeandikwa: Elizabeth Zaya, Beatrice Shayo, Beatrice Moses (Dar) na Francis Godwin (Iringa)***

## HABARI KITAIFA

# Wahusika kifo cha mtangazaji ITV wasakwa

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kinondoni, limesema linaendelea na uchunguzi ili kubaini waliohusika na mauaji ya aliyekuwa mwandishi wa habari wa ITV/Redio One na mtayarishaji wa kipindi cha Jarida la Wanawake ITV, Blandina Sembu (47).

Kamanda wa Polisi mkoa humo, Ramadhani Kingai, akizungumza na Nipashe jana, alisema uchunguzi bado unaendelea kubaini wahusika wa tukio hilo.

Taarifa iliyotolewa na jeshi hilo juzi, ilisema Blandina aliuawa Machi 27, mwaka huu baada ya kupigwa na kitu chenye ncha kali usoni, huku mwili wake ukikutwa Bamaga-ITV, Mwenge, jijini Dar es Salaam. Kamanda Kingai alisema mwili wa Blandina uliokotwa eneo la Maryland Bar, njia panda ya ITV, huku watu wasiofahamika wakiwa na gari aina ya Noah, ambalo halijatambuliwa namba, wakitajwa kuhusika.

"Walisimamisha gari eneo hilo, kwa muda mfupi na lilipoondoka ulipatikana mwili wa jinsia ya kike, alitambulika kuwa ni Blandina mfanyakazi wa ITV, Redio One," alisema Kamanda Kingai.

"Eneo alikookotwa ni Area B, alikouliwa ni kwingine, sababu mwili ulionekana muda mfupi tu eneo la Bamaga, hivyo uchunguzi unaendelea."

Kamanda huyo alifafanua kuwa, marehemu alikuwa ni mkazi wa Zinga, Bagamoyo mkoani Pwani.

### LHRC CHALAANI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimesema kimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Blandina na upelelezi wa tukio hilo ufanyike ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria, ili wananchi waheshimu haki za binadamu na kuwa walinzi wa haki ya kuishi.

LHRC ilisema ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasema kwamba, kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI,VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI
(OSHA)



Bodi ya Ushauri (MAB),Menejimenti na Watumishi wote wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), wanaungana na Watanzania wote kutoa salamu za pongezi kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)
PO Box 519, Dar es Salaam
Nukushi +255-22-2760552 | Simu: +255-22-2760548
Barua pepe: info@osha.go.tz

Osha_tanzania_official | Occupational Safety And Health Authority | Tanzaniaosha | Osha Tv Online


# Shule 7 kufundisha tahasusi mpya 5

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ametangaza shule saba za sekondari zitakazofundisha tahasusi (combination) mpya tano kwa ajili ya wanafunzi wanaoingia kidato cha tano mwaka huu ili kuondoa tatizo la ukosefu wa wataalamu nchini.

Shule hizo ni Shule ya Sekondari ya Wasichana Dodoma, Morogoro, Makambako, na Shule ya Ufundi ya Wavulana Iyunga, Usagara, Kibiti na Mpwapwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa, Waziri Jafo alitaja tahasusi hizo kuwa ni Physics, Mathematics na Computer Studies (PMC),Kiswahili, French, Chinese (KFC), Kiswahili, English, Chinese (KEC), Physical Education, Biology, Fine Art (PeBFa) na Physical Education, Geography, Economics (PeGE).

Alifafanua kuwa tahasusi ya PMC itatolewa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Dodoma na Shule ya Sekondari ya wavulana ya Iyunga.

Aidha, alisema tahasusi ya KFC na KEC itatolewa katika Shule ya Sekondari ya wasichana Morogoro na ya wavulana Usagara na tahasusi ya PBF na PGE itatolewa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Makambako, Shule ya Sekondari ya wavulana Kibiti na Sekondari ya Mpwapwa ambayo ni ya mchanganyiko.

"Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa fursa kwa wahitimu kubadili machanguo yao ili kuwawezesha wanafunzi kusoma fani au tahasusi itakayomwandaa kuwa na utaalamu fulani katika maisha yake ya baadaye kwa namna ambayo anatamani yeye mwenyewe au kwa kushauriawa na wazazi wake," alisema.

Alisema nchi ilikosa kuwa na wataalamu wa michezo kutokana na kutokuwapo na tahasusi maalum, hivyo hatua hiyo itasaidia upatikanaji wake.

Waziri Jafo alisema ratiba ya kubadili inaanza Machi 29 hadi Aprili 11, 2021 ambapo wanafunzi wataingia kwenye mtandao na kutumia namba zao za mitihani ya 2020 kisha mfumo utawaelekeza kwa hatua zote.

"Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wanafunzi hawakujaza kwa uhakika tahasusi au kozi zao kutokana na kutokuwa na uhakika wa ufaulu katika masomo yao," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa wanafunzi hao wanafahamu walivyofaulu na kwa sababu hiyo watachagua tahasusi au fani za kusomea kwa uhakika sawa na viwango vyao vya ufaulu.

Hata hivyo, alisema baada ya muda huo kupita, hakutakuwa na nafasi ya kufanya uchaguzi mwingine tena, isipokuwa taarifa za awali ndizo zitakazotumika.

## TANGAZO

# MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC

## New Rates-VAT Exclusive, Effective dates APRIL 1, 2021 Toll-free: 0800 750 040

| Tariff | Current a/c Business - Sole propriator, Companies | Community Current A/C | Current A/C Personal | Call A/C | Savings Business | Savings Diocese, Parish, Jumuiya | Savings Personal | Bishop A/C | Integrity A/C | Student A/C | Joint/ Wanandoa A/C | Mwana A/C | Wajasiriamali A/C | Forex A/C | Salary A/C | Vicoba/Informal Group A/C | Priest A/C | Nun A/C |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening amount | 100,000 | 20,000 | 15,000 | 5,000,000 | 50,000 | 20,000 | 15,000 | 50,000 | 20,000 | 5,000 | 30,000 | 15,000 | 16,000 | $/€/£ 100 | zero | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 | 10,000 | 20,000 | 5,000,000 | 20,000 | 10,000 | 10,000 | 50,000 | 10,000 | zero | 10,000 | 5,000 | 10,000 | $/€/£ 50 | zero | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| Interest rate payable below 5m | n/a | n/a | n/a | n/a | 0.5% | n/a | 0.5% | n/a | up to 2% | 0.5% | 0.5% | 0.5% | 0.5% | n/a | n/a | 0.50% | n/a | n/a |
| Interest rate payable above 5m | n/a | n/a | n/a | up to 4% | 2.0% | n/a | 2.0% | n/a | up to 5% | 2.0% | 2.0% | 2.0% | 2.0% | n/a | n/a | 1.00% | n/a | n/a |
| Interest minimum earning balance | n/a | n/a | n/a | 5,000,000 | 100,000 | n/a | 100,000 | n/a | 500,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 | n/a | n/a | 100,000 | n/a | n/a |
| Monthly maintanance fee | 12,000 | free | 10,000 | free | 1,500 | free | 1,500 | free | free | free | 2,000 | free | free | free | n/a | free | free | free |
| Deposit fee (Notes) | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free |
| Deposit fee(Coins) | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| Teller withdraw fee below 5m | 4,000 | free | 4,000 | free | 4,000 | Free | 4,000 | free | free | 1,500 | 4,000 | 4,000 | free | 0.1% min $/€/£ 2 max 50 | free | free | 3,000 | 3,000 |
| Teller withdraw fee below 5m - 20m | 6,000 | free | 6,000 | free | 6,000 | free | 6,000 | free | free | 5,000 | 6,000 | 6,000 | free | | free | free | 3,000 | 3,000 |
| Teller withdraw fee above 20m | 0.12% max 100,000 | free | 0.12% max 100,000 | free | 0.12% max 100,000 | free | 0.12% max 100,000 | free | free | 0.12% max 100,000 | 0.12% max 100,001 | 0.12% max 100,002 | 0.12% max 100,003 | | free | free | 3,000 | 3,000 |
| Teller B/E | 500 | 500 | 500 | free | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 | 500 |
| Monthly statement | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free |
| Adhock statement | 1,500 | 1,500 | 1,500 | free | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | $/€/£ 1.5 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Other charges** | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Certificate of Balance | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | $/€/£ 15 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Confirmation to Auditors | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | $/€/£ 15 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Search for information over 5 years | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | $/€/£ 15 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Cheque book costs (per leaf) | 500 | free | 500 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 0.25 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| Bankers cheque issued (BP's) | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 15 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| Status Report | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 12 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| Stop payment | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 15 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| Dishonored Cheque for lack of funds or refer to drawer or effects not cleared | 150,000 | 150,000 | 150,000 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 50 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| Dishonored Cheque due to techinical error caused by customer | 30,000 | 30,000 | 30,000 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 15 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| Dormant account activation | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free | free |
| Closing account less than six month (other than SGL accounts) | 30,000 | 30,000 | 30,000 | n/a | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | $/€/£ 15 | n/a | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Counter cheque book per leaf | 10,000 | 10,000 | 10,000 | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 15 | n/a | n/a | n/a | n/a |
| monthly Charge drawn below Minimum balance | 10,000 | 10,000 | 10,000 | n/a | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | $2 /€1.5 /£1.5 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| Salary processing/bulk payment (per entry) | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | $/€/£ 1 | 2,000 | n/a | n/a | n/a |
| **(a) Standing order** | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| (i) Instructions within Mkombozi bank | 5,000 | 5,000 | 5,000 | n/a | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | $/€/£ 3 | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| (ii) Standing orders to other banks | 15,000 | 15,000 | 15,000 | n/a | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | n/a | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| (iii) Unpaid bankers orders | 30,000 | 30,000 | 30,000 | n/a | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | $/€/£ 15 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| **(b) Mobile banking charges** | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| (i) Transfer from Bank to MNOs | n/a | n/a | YES | n/a | n/a | n/a | YES | YES | n/a | YES | n/a | n/a | YES | n/a | YES | n/a | YES | YES |
| 1,000-50,000 | | | 1,000 | n/a | n/a | n/a | 1,000 | 1,000 | n/a | 1,000 | n/a | n/a | 1,000 | n/a | 1,000 | n/a | 1,000 | 1,000 |
| 50,001-100,000 | | | 1,500 | n/a | n/a | n/a | 1,500 | 1,500 | n/a | 1,500 | n/a | n/a | 1,500 | n/a | 1,500 | n/a | 1,500 | 1,500 |
| 100,001-300,000 | | | 2,000 | n/a | n/a | n/a | 2,000 | 2,000 | n/a | 2,000 | n/a | n/a | 2,000 | n/a | 2,000 | n/a | 2,000 | 2,000 |
| 300,001-500,000 | | | 3,000 | n/a | n/a | n/a | 3,000 | 3,000 | n/a | 3,000 | n/a | n/a | 3,000 | n/a | 3,000 | n/a | 3,000 | 3,000 |
| 500,001-1,000,000 | | | 4,000 | n/a | n/a | n/a | 4,000 | 4,000 | n/a | 4,000 | n/a | n/a | 4,000 | n/a | 4,000 | n/a | 4,000 | 4,000 |
| 1000001-1,500,000 | | | 5,000 | n/a | n/a | n/a | 5,000 | 5,000 | n/a | 5,000 | n/a | n/a | 5,000 | n/a | 5,000 | n/a | 5,000 | 5,000 |
| 1,500,001-3,000,000 | | | 6,000 | n/a | n/a | n/a | 6,000 | 6,000 | n/a | 6,000 | n/a | n/a | 6,000 | n/a | 6,000 | n/a | 6,000 | 6,000 |
| (ii) Internal Bank Account Transafer | | | 500 | n/a | n/a | n/a | 500 | 500 | n/a | 500 | n/a | n/a | 500 | n/a | 500 | | 500 | 500 |
| (ii) Transfer from MNOs to Bank | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | | n/a | n/a |
| (iii) Balance Enquiry | n/a | n/a | 300 | n/a | n/a | n/a | 300 | 300 | n/a | 300 | n/a | n/a | 300 | n/a | 300 | n/a | 300 | 300 |
| (iv) Mini statement | n/a | n/a | 500 | n/a | n/a | n/a | 500 | 500 | n/a | 500 | n/a | n/a | 500 | n/a | 500 | n/a | 500 | 500 |
| **(c) EFT / SWIFT / TISS transfers** | | | | n/a | | | | | | | | | | | | | | |
| (i) EFT Within the bank (Incoming) | free | free | free | n/a | free | free | free | free | free | free | free | free | free | n/a | free | free | free | free |
| (ii) EFT to other banks | 1,500 | 1,500 | 1,500 | n/a | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | n/a | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| (iii) TISS transfers | 10,000 | 10,000 | 10,000 | n/a | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | n/a | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| (iii) Swift transfers | USD 50 plus swift charges | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| **ATM & ID Cards charges** | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Customer ID | n/a | n/a | n/a | 12000 | 12000 | 12,000 | n/a | n/a | 12,000 | n/a | 12,000 | 12,000 | n/a | $/€/£ 5 | 12,000 | 12,000 | n/a | n/a |
| New ATM Card | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | 5,000 | 5,000 | n/a | 5,000 | n/a | n/a | 5,000 | n/a | 5,000 | n/a | 5,000 | 5,000 |
| Replacement of lost/ damaged ATM card | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | 10,000 | 10,000 | n/a | 10,000 | n/a | n/a | 10,000 | n/a | 10,000 | n/a | 10,000 | 10,000 |
| ATM Monthly fee per month (charged quarterly or annually) | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | 500 | 500 | n/a | 500 | n/a | n/a | 500 | n/a | 500 | n/a | 500 | 500 |
| ATM Balance inquiry | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | 200 | 200 | n/a | 200 | n/a | n/a | 200 | n/a | 200 | n/a | 200 | 200 |
| ATM Withdraw charges per transaction | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | n/a | 1,300 | 1,300 | n/a | 1,300 | n/a | n/a | 1,300 | n/a | 1,300 | n/a | 1,300 | 1,300 |

| **Fixed deposit rates - Local currency** | | **Fixed deposit rates - Forex (USD)** | | **Fixed deposit rates - Forex (EURO)** | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 months | 4% p.a | 30 Days | 0.305% p.a | 30 Days | 0.00% p.a |
| 6 months | 5% p.a | 60 Days | 0.65% p.a | 60 Days | 0.00% p.a |
| 9 months | 6% p.a | 90 Days | 1.10% p.a | 90 Days | 0.00% p.a |
| 12 months | 7% p.a | 180 Days | 1.15% p.a | 180 Days | 0.00% p.a |
| 18 months | 8% p.a | 360 Days | 1.35% p.a | 360 Days | 0.00% p.a |
| 24 months | 9% p.a | Above USD 100,000 | negotiable | Above USD 100,000 | negotiable |
| 36 months | 10%p.a | | | | |
| Above TZS 100 Million | Negotiable | | | | |
| Premature Closure penalty | 50% of accrued Interest foregone | Premature Closure penalty | 50% of accrued Interest foregone | Premature Closure penalty | 50% of accrued Interest foregone |
| After maturity without notice from Client | Upon FDR maturity without any notice from Client to the Bank, there shall be an automatic rollover/renewal of the particular FDR basing on the prevailing board rates in the same tenure/period the same have had before. | After maturity without notice from Client | Upon FDR maturity without any notice from Client to the Bank, there shall be an automatic rollover/renewal of the particular FDR basing on the prevailing board rates in the same tenure/period the same have had before. | After maturity without notice from Client | Upon FDR maturity without any notice from Client to the Bank, there shall be an automatic rollover/renewal of the particular FDR basing on the prevailing board rates in the same tenure/period the same have had before. |

| ***Loans**** | ***Agriculture*** | ***Business*** | ***Housing Microfinance*** | ***InsurancePremium Financing*** | ***Mortgage*** | ***Salaried*** | ***SGL*** | ***OD*** | ***Wastaafu*** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Interest Rate | 17%p.a | 26% p.a | 25%p.a | 19%p.a | 18%p.a | 18%p.a | 39%p.a | 25%p.a | 18%p.a |
| Processing Fee | 1%flat | 2.5%flat | 2.5%flat | N/A | 2.5%flat | 2.5%flat | 2.5%flat | 2.5%flat | 1%flat |
| Insuarance Fee | 0.1% per month | 0.1% per month | 0.1% per month | N/A | 0.1% per month | 2%flat on the disbursed amount for Public Sector and 1.2%pa of the loan amount payable upfront for the tenor of facility for Private Sector | 0.1% per month | 0.1% per month | 2% On the disbursed amount |
| Mortgage Fee | 1%flat | 1%flat | 1%flat | N/A | 1%flat | N/A | N/A | 1.2%flat | N/A |
| Discharge Fee | Tzs.80,000/ | Tzs.80,000/ | Tzs.80,000/ | N/A | Tzs.80,000/ | Tzs.80,000/ | N/A | Tzs.80,000/ | N/A |
| Penalties | 13%p.a | 22%p.a | 21%p.a | 15%p.a | 23%p.a | N/A | 35%p.a | 30%p.a | N/A |

***Loan Interest rates are indicative. The actual pricing shall depend on the type and risk level of the underying client and business.**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ripoti ya CAG imeonyesha uhalisi

**JUZI** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), aliweka hadharani baadhi ya madudu yaliyopo kwenye Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na mashirika ya umma kwa kuonyesha mchwa wanaoendelea kulitafuna taifa pamoja na hasara kubwa iliyopo.

Mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, CAG alibainisha kuna ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni 3.6 katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kujiendesha kwa hasara na mwaka jana pekee kupata hasara ya Sh. bilioni 60, na kwa miaka mitano likitengeneza hasara.

Aidha, alibainisha mchwa waliopo kwenye halmashauri nchini ikiwamo kushindwa kutumia mifumo sahihi ya Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA), jambo lililosababisha mapato mengi kuzidi kupotea.

Pia ilionekana dosari kwenye mashirika ya umma ambayo hayafanyi vizuri kiasi cha kupata hati chafu, jambo lililomlazimu Rais Samia kumwagiza CAG kuweka wazi taasisi na mashirika husika ili hatua zaidi zichukuliwe.

Ripoti hizi ni za kitaalamu ambazo ofisi ya CAG inazifanyia kazi kwa uchunguzi wa kina, na zitawekwa bayana baada ya kuwasilishwa bungeni wiki hii na ndipo mbivu na mbichi zitajulikana, lakini juzi kwa uchache ilionekana picha halisi.

Zimekuwa zikiwasilishwa na kuonyesha madudu mengi ambayo yanahitaji wahusika kuwajibika moja kwa moja, ili kuokoa fedha za umma ambazo zingetumika kuboresha huduma za jamii kama afya, elimu na miundombinu.

Kati ya maneno yaliyoguswa na CAG lipo eneo la serikali za mitaa ambalo baadhi ya halmashauri zimepata hati chafu na ni tatizo linalojirudia mara kwa mara tangu utawala wa awamu ya tatu na awamu ya nne.

Halmashauri zinapokea fedha nyingi kutoka serikali kuu na kupitia shughuli zake mbalimbali, inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, huku kukiwa na uwakilishi wa moja kwa moja wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Tayari Rais ameshatoa maelekezo ya kusimamishwa kazi kwa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, kupisha uchunguzi huku akimwagiza Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuchukua hatua kwa ubadhirifu uliobainishwa na CAG.

Aidha, Waziri wa TAMISEMI ameagiza kuchukuliwa hatua kwa wakaguzi wa ndani na waweka hazina wa halmashauri nane zilizopata hati chafu, huku akipeleka majina ya wakurugenzi wa halmashauri hizo kwa rais ambaye ndiye mamlaka ya uteuzi.

Ni matumaini yetu kuwa ripoti hizo zitafanyiwa kazi na kutakuwa na uwajibikaji wa kina kwa kila aliyehusika kwa namna moja au nyingine kusababisha hasara kubwa.

Tunatarajia kuona uwajibikaji na kurudishwa kwa fedha za umma, lakini uhalisia kwenye mashirika ya umma ambayo kwa uendeshaji wake yamegeuka kuwa mchwa anayetafuna fedha za umma ambazo zingetumika kwenye miradi ya maendeleo inayogusa maisha ya watu moja kwa moja.

Watanzania wanataka kuona uwajibikaji, wanataka kuona fedha zao zinatumiwa ipasavyo kwa kuwa bado wana mahitaji ya msingi kama ya zahanati, vituo vya afya, vifaa tiba, dawa, miundombiu ya elimu na huduma za maji, ambazo huenda wamezikosa kutokana na kukosa fedha za kugharamia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wadau wote elimu wahusike katika ujenzi maktaba shule

Na Sabato Kasika

**MAKTABA** za shule zinatajwa kuwa kiungo muhimu katika kukamilisha malengo ya elimu ya msingi na sekondari, ambazo humtayarisha mwanafunzi kuwa raia bora katika jamii yake na taifa kwa ujumla.

Vilevile, maktaba inamwezesha na kumkuza mtumiaji kuwa na tabia ya kuendelea kujifunza, uwezo wa kutafiti, kudadisi, kubuni, kuhoji, kuchambua na kutathmini hali ya mambo, ili kumfikisha katika uamuzi sahihi.

Kama ilivyo kwingineko, maktaba za shule zinapaswa kuwa na mkusanyiko wa vitabu vya ziada na kiada kwa masomo yote, vitabu rejea, muhtasari ya masomo, atlasi, vitabu vya hadithi, kazi zilizofanywa na wanafunzi, karatasi za mitihani iliyopita na ramani mbalimbali duniani.

Bado kuna upungufu, shule nyingi za msingi na sekondari hazina huduma hiyo, hali inayosababisha wanafunzi kukosa sehemu ya kwenda kujisomea, hivyo kukosa sehemu ya kujiongezea ujuzi na uelewa kwa wakati wake kwa kutumia nyenzo hiyo ya shule.

Nikiri, serikali imekuwa ikiboresha miundombinu ya shule za umma hasa za msingi na sekondari, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maktaba madarasa, pia majengo kwa ajili ya maabara.

Juhudi hizo ni nzuri na za kuungwa mkono, lakini ikiwezekana, kasi ya ujenzi wa maktaba za kisasa na ununuzi wa vitabu mbalimbali kwa ajili ya shule za umma ingeongezwa zaidi.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, maarifa yamejificha katika vitabu, ambavyo kama vitakuwapo vya kutosha katika maktaba na wanafunzi wakajisomea, watajiongezea uelewa wa mambo mbalimbali.

Maktaba ni sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kujisomea, kujifunza kwa njia ya kusoma maandiko katika vitabu na machapisho mbalimbali kwa lengo ya kujiongezea ujuzi au uelewa.

Vitabu na machapisho yaliyomo kwenye maktaba, yanalenga kuongoza uelewa, maarifa na ujuzi kwa wasomaji na hasa wanafunzi, hasa kupitia vitabu wa kiada na ziada.

Kimsingi, mwanafunzi anapomaliza kufundishwa na mwalimu darasani, ni muhimu atenge muda wa kwenda maktaba kujisomea vitabu vinavyoendana na kile alichofundishwa darasani, ili kupanua wigo wa uelewa kwa kutumia vitabu mbalimbali vya marejeo.

Hivyo, mwanafunzi kutegemea tu 'notisi' za mwalimu wake bila kutafuta njia nyingine ya kujisomea na hasa kwenye maktaba, hawezi kuwa na maarifa ya kujitosheleza na pia atakosa na ujuzi na uelewa zaidi wa vitabu mbalimbali.

Kwa muda mrefu sasa, serikali imekuwa ikiboresha miundombinu ya shule za umma hasa za msingi na sekondari, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa, majengo kwa ajili ya maabara na pia maktaba.

Hivyo, suala la kuwapo kwa maktaba katika shule ni jambo la msingi, ambalo wadau wote wa elimu wakiwamo wazazi, ni vyema wakashiriki kwa hali na mali kuhakikisha shule za umma zinakuwa na huduma hiyo.

Wapo baadhi ya wadau ambao wameonyesha mfano wakiwamo wa wilaya ya Musoma mkoani Mara, ambao sasa wanashirikiana na serikali katika ujenzi wa maktaba katika shule zote 111 za msingi na 22 za sekondari.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Vincent Anney, nguvukazi yao inatumika kusoma, maji, mchanga, mawe na kokoto, kufanikisha ujenzi huo na kwamba wanataka kuhakikisha shule zote zinakuwa na maktaba.

Katika maelezo yake, mkuu huyo wa wilaya, anasema wapo wafadhili wanaosaidia upatikanaji wa vitabu na samani za maktaba, ili kusaidia wanafunzi na watu wengine kujisomea katika mazingira safi.

Pamoja na ujenzi huo, ipo pia haja ya kuhamasisha watu kutambua umuhimu wa kujisomea ili kutenga muda wa kwenda katika maktaba ambazo zimeanza kufanya kazi ili wawe wanasoma vitabu na machapisho mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# Mtuhumiwa wa ujambazi auawa akipambana na polisi

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

MTU mmoja anayesadikiwa kuwa jambazi ameuawa katika majibizano ya risasi na polisi na wengine watano kukimbia katika eneo la Kagerankanda, wilayani Kasulu, mkoani Kigoma, juzi usiku.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Charles Manyama, alisema polisi walipata taarifa toka kwa raia wema kuwa kuna kundi la watu sita wenye silaha katika eneo hilo na polisi waliokuwa doria walikwenda kukabiliana nao.

Alisema katika majibizano ya risasi mtu mmoja ambaye hajatambulika alijeruhiwa na kufariki baadaye wakati akikimbizwa hospitali huku wenzake watano wakifanikiwa kukimbia.

Kamanda alisema marehemu alikutwa na bunduki moja ya kivita aina ya AK 47 na magazine yenye risasi 17 katika eneo la tukio.

Kamanda Manyama alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu kwa uchunguzi na utambuzi na msako mkali kwa waliokimbia, amewaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo.

Kutokana na tukio hilo baadhi ya wananchi wameliomba Jeshi la Polisi kuongeza ulinzi katika maeneo hatarishi hasa katika barabara ya Kasulu-Kibondo na Kasulu-Kagerankanda ili kukomesha matukio ya uhalifu.

# Sekta ya madini yaingiza bil. 400/- miezi minane

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema ndani ya miezi minane serikali imekusanya Sh. bilioni 399.09 kupitia sekta ya madini nchini.

Biteko aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu hoja kwenye kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Alisema sekta hiyo imezidi kuimarika miaka ya hivi karibuni kutokana na juhudi za serikali ikiwamo kuanzisha na kusimamia masoko na vituo vya kuuzia madini katika maeneo yote yanapopatikana madini nchini.

"Kasi ya ukusanyaji na mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa umeongezeka ambapo katika kipindi cha Julai 2020 mpaka Februari 2021, serikali ilikusanya jumla ya Sh. bilioni 399.09 sawa na asilimia 113.73 ya lengo ya makusanyo kwa kipindi husika," alisema.

Waziri Biteko alisema kuwa, juhudi za kuanzisha na kusimamia masoko na vituo vya madini imesaidia kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya serikali, mapato yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Alisema katika kipindi cha robo tatu ya mwaka 2020 mchango wa Sekta ya Madini umekuwa kwa asilimia 6.4 na lengo la wizara ni kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025.

Naye Katibu Mkuu Wizara hiyo, Prof. Simon Msanjila, alisema wizara imeshaandaa timu ili kuanza kuandaa utekelezaji wa kituo cha utalii wa madini na yanayopatikana nchini yataonyeshwa hapo ili kuongeza mapato yatokanayo na rasilimali hiyo.

Hata hivyo, alisema katika kudhibiti utoroshaji wa madini ya dhahabu wizara imesajili mialo yote ili kuhakikisha kiasi kinachozalishwa katika kila mwalo kinapelekwa kuuzwa katika masoko ya madini yaliopo nchini.



Kinamama wakichimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa maktaba ya Shule ya Msingi Karubugu iliyopo Kata ya Mugango, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, juzi ikiwa ni kuchangia nguvu kazi yao katika uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ummy: Hoja 15 za Muungano zimepatiwa ufumbuzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu, amesema hoja 15 kati ya 25 za Muungano zilizosajiliwa, zimepatiwa ufumbuzi huku 10 zilikiwa kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi.

Mwalimu aliyasema hayo jana alipokuwa akiwasilisha taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

"Kupitia vikao vya pamoja baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jumla ya hoja 25 zilisajiliwa na kati ya hizo hoja 15 zimepatiwa ufumbuzi, 10 ziko katika ngazi mbalimbali za maamuzi," alisema.

Alisema serikali zitahakikisha kero zinazojitokeza zinapatiwa ufumbuzi mapema kwa mustakabali endelevu wa Muungano.

"Serikali itaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto za Muungano kadiri zinavyojitokeza na kuhakikisha hoja za Muungano ambazo zimepatiwa ufumbuzi maazimio na makubaliano yake yanatekelezwa na pande zote mbili za Muungano," alisema.

Alitaja mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 kuwa ni pamoja na kuratibu vikao vya kamati ya pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano, kikao cha kusaini hati tano za makubaliano ya kuondoa kwenye orodha ya hoja za Muungano, hoja zilizopatiwa ufumbuzi kilichofanyika Oktoba 17, mwaka 2020, jijini Dar es Salaam.

Aidha, alisema katika kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii, taasisi 12 zilitembelewa Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Muungano na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande hizo mbili.

"Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo vikao saba vya ushirikiano vilifanyika," alisema.

Akizungumzia mwaka wa fedha ujao, alisema ofisi yake itaweka mkazo katika kutatua kero za Muungano hususan masuala ya fedha, kuimarisha ushirikiano kwa taasisi zisizo za Muungano zenye sekta zinazoshabihiana na kutolea mfano sekta za afya, elimu na mawasiliano.

Alisema kuwa SMT na SMZ zitaendelea kushirikiana katika kuibua miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo hufadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa manufaa ya wananchi wa pande mbili za Muungano.

"Miradi ambayo imewasaidia wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki na kuinua hali zao za kiuchumi pamoja na kuongeza ajira kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria, Mohammed Mchengerwa, alishauri serikali kuendelea kutoa elimu hususan kwa vijana waliozaliwa baada ya Muungano kuelezea fursa na faida zake.

# Wananchi Chato waingia wasiwasi kuondoka JPM

**Na Richard Makore,** aliyekuwa CHATO

SIKU nne baada ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati John Magufuli kuzikwa kijijini kwake wilayani Chato, mkoani Geita, baadhi ya wananchi wilayani humo wameonyesha wasiwasi wao kama mji huo utaendelea kukua kibiashara kama ilivyokuwa awali.

Miongoni mwa vitu vilivyovutia wafanyabiashara wengi kuwekeza Chato ni pamoja na kuwapo miundombinu mizuri ya barabara, umeme, maji, elimu, afya pamoja na jina la Magufuli.

Baadhi ya wafanyabiashara hao walisema jina la Magufuli lilivuta watu wengi kuwekeza Chato tangu alipoingia madarakani mwaka 1995.

Mfanyabiashara wa nyumba za kulala wageni, Mwita Chacha, alisema mji wa Chato ulianza kukua kidogo kidogo, lakini kasi iliongezeka baada ya Hayati Magufuli kuchaguliwa kuwa mbunge mwaka 1995.

Alisema hapo awali Chato ilikuwa Jimbo la Bihalamulo Mashariki, kabla ya eneo hilo kugawanywa na kupatikana jimbo hilo ambalo Hayati Magufuli aliendelea kuliwakilisha.

Chacha alisema baada ya Hayati Magufuli kupata ubunge alipeleka maendeleo ya haraka katika jimbo hilo ikiwamo kujenga barabara, maji, elimu na afya.

Hata hivyo, Chacha alisema watu wengi walikuwa wanakwenda Chato kuwekeza kutokana na jina la Magufuli huku wakiamini mji huo ungeendelea kukua.

Alisema baada ya Magufuli kuwa rais wa awamu ya tano, watu wengi waliongezeka mjini Chato ambao walitoka maeneo mbalimbali ya nchi ikiwamo mikoa ya jirani.

Mfanyabiashara wa chakula mjini Chato, Clory Daudi, alisema tangu ulipotangazwa msiba wa Hayati Magufuli watu waliongezeka mjini humo ghafla.

Alisema wananchi hao walichangia kufanya biashara ya chakula usiku na mchana na licha ya bei kuongezeka, walifanya biashara.

Glory alisema anaamini wafanyabiashara wengi hasa wakubwa walikuwa wanawekeza Chato kutokana na jina la Hayati Magufuli ambalo nyuma yake lilibeba watu wengi.

Akizungumzia maisha ya Chato baada ya Hayati Magufuli, mbunge wa jimbo hilo, Medard Kalemani, aliwataka wananchi kushikamana na kuendelea eneo hilo.

"Chato itaendelea kuwa imara sana kesho, sasa na kuliko jana na nawaomba wana Chato tumuenzi Hayati Magufuli kwa kudumisha mshikamano wetu," alisema.

Kalemani aliwahakikisha wananchi wa Chato kwamba miradi iliyoanzishwa itamalizika ili kutimiza ndoto za Hayati Magufuli ambazo alikuwa akiziota wakati wa uhai akiwa rais.



Watuhumiwa wa kosa la kukutwa na nyara za serikali ikiwamo ngozi ya chui, zenye thamani ya Sh. milioni 8, Adam Mohamed (wa pili kushoto) na mwenzake, Nganya Mkanyagae, wakisindikizwa na Polisi kuingi katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, jana, kusikiliza kesi inayowakabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wamtaka CAG kukagua ujenzi jengo h/shauri

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAKAZI wilayani Tarime mkoani Mara hususani wa Halmashauri ya Mji Tarime, wamemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo na Katibu Mkuu TAMISEMI, Joseph Nyamhanga, kutuma wakaguzi kufuatilia matumizi ya Sh.1,538,932,264.21 kati ya Sh. 3,115,458,992.30 zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Mji Tarime.

Wametoa ombi hilo kutokana na madai ya kukwama kwa ujenzi huo eneo la Bomani.

Wakizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki baadhi ya wakazi wa Mji wa Tarime waliojitambulisha kwa majina Maiko Marwa, Matiko Samwel, Rose Otieno, Wambura Chomete, Rugumba Mairo, Alois Gitinkwi na Magaigwa Charles, walisema kuwa wananchi hususani wa Halmashauri ya Mji Tarime wamesikitishwa kukwama ujenzi wa jengo la ghorofa kwa zaidi ya miezi 8 tangu mwaka jana na jengo hilo kwa sasa limezungukwa na vichaka, huku ikidaiwa shilingi bilioni 1.5 kutumika katika ujenzi huo.

Waliomba wakague pia ujenzi wa kituo cha mafuta kinachojengwa katikati ya makazi na eneo dogo ambalo eneo hilo kulikuwa na jengo kubwa la Halmashauri lililokuwa na vyumba vingi ambavyo wapangaji walikuwa wakilipa halmashauri mamilioni ya fedha, lakini wamebadilisha matumizi ya awali ya kujenga ghorofa kwa ajili ya maduka.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Tarime, Daniel Komote, alisema kuwa ujenzi wa jengo la ghorofa la Halmashauri eneo la Bomani ulianza Aprili 10, 2017 na mkandarasi alikuwa Wakala wa Majengo (TBA) ambapo Aprili 10, 2017 mkandarasi huyo alilipwa Sh. 500,000,000 hati ya pili mwaka 2018 alilipwa Sh. 325, 145, 912.72 malipo mengine yalifanyika Oktoba 8, 2018 ya Sh. 152,702,369.93.

# Kibano chaja abiria wasiofunga mikanda

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JESHI la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma linaandaa utaratibu wa kuanza operesheni za kuwakamata na kuwatoza faini abiria ambao watabainika kusafiri kwenye magari wakiwa wamesimama na kutofunga mikanda.

Sambamba na abiria hao, pia kadhia ya aina hiyo itawakumba abiria na madereva watakaosafari na pikipiki bila kuvaa kofia ngumu, ukiwa ni utekelezaji wa idara hiyo kukabiliana na ajali za barabarani kwenye wilaya yao.

Maelekezo hayo yametolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani, Athumn Nkinde, wakati akifunga kikao cha wajumbe wa Kamati ya Usalama Barabarani wilayani hapa.

Alisema kinachosubiriwa sasa ni ukamilishaji wa mafunzo kwa madereva kulingana na maelekezo yaliyotolewa na serikali wilayani humo.

Nkinde aalisema maamuzi hayo yamefikiwa baada ya kubaini uwapo wa kundi kubwa la abiria ambao wamekuwa wakisafiri kutozingatia na kutii maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa na wamiliki, wahudumu na madereva wa vyombo husika kwa kutoa visingizio ambavyo vimekuwa vikiwagharimu wamiliki wa magari na pikipiki kulipa faini sisizowahusu.

Mmoja wa wajumbe, Rajab Mkwawa Mtimbalugono, alihoji kama serikali ilivyojipanga kuwanusuru hasa abiria wa pikipiki na magonjwa ya ngozi yatakayotokana na watu wengi kuchangia uvaaji wa kofia moja.

Wakitoa uzoefu wa majeruhi ambao hupokelewa hospitalini, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya, Dk. Wendy Robert na mteknolojia wa mionzi wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru, Emmnuel Nzige, walisema majeruhi wengi hufika wakiwa wameumia vibaya sehemu za vichwa, hivyo madhara ambayo hutokana na ajali hizo ni kubwa mno ikilinganishwa na sababu ambazo hutolewa ili kukwepa kuvaa kofia ngumu na kufunga mikanda ndani ya magari.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Tunduru, Anosisye Mwaipopo, alisema kuwa kwa waendesha pikipiki sharti ni kuvaa kofia ngumu kwa dereva na abiria wake.

HABARI KITAIFA

# Kinamama wawakwepa wenza wao kutumia uzazi wa mpango

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WANAWAKE wengi walio kwenye ndoa wanalazimika kuacha kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kutumia njia za uzazi wa mpango na kutumia njia ambazo wenza wao hawataweza kuzibaini.

Akielezea hali hiyo Mganga Mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Robert Rwebangira, alisema wamebaini wanawake wengi kutumia njia ya sindano au vidonge kama hatua ya kuficha kubainika kujihusisha na matumizi hayo.

Rwebangira alieleza aina hiyo ya kupanga uzazi inapaswa kutumika kwa muda ufupi kati ya miezi sita na isizidi miaka miwili, tofauti na hapo inaweza msababishia mwanamke kupata maudhi madogo madogo pamoja na hatari ya kuchelewa au kushindwa kupata ujauzito.

"Wanawake wengi wanatumia njia za muda mfupi kwa kipindi kirefu, hiyo ni hatari na ni mbaya kwa afya ya uzazi," alisema.

Mwanaume mmoja kwa sharti la kutokutajwa jina, alilieleza gazeti hili kuwa hakubaliani na matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango, lakini baadaye alibaini mwenza wake anatumia njia ya sindano kwa siri.

"Sikuwa tayari mke wangu ajiingize kwenye matumizi hayo, lakini naona baada ya kuzaa watoto wawili mfululizo akajiongeza pasipo ruhusa yangu," alisema.



Mwalimu James Eliamani Mmbando (kulia), akimkabidhi kiti choo (Commode Chair) mmoja wa wazee wenye mahitaji maalumu wanaotunzwa katika Makazi ya Wazee wasiojiweza Miembeni, Manispaa ya Moshi. Mmbando kwa kushirikiana na marafiki zake akiwamo Franziska Aadler kutoka Ujerumani wamejitolea mablanketi, mashuka, masweta, soksi, vyakula vya aina mbalimbali, sabuni, na mahitaji mengine mbalimbali yenye thamani ya zaidi ya milioni nne. PICHA: JAMES LANKA

# Wazazi, walezi waelezwa mwarobaini wa utapiamlo

**Na Restuta Damian,** KARAGWE

WAZAZI na walezi wa vijiji vya Nyakagoyagoye na Nyamweli Kata ya Kiluluma Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, wameshauriwa kutumia vyakula wanavyozalisha shambani na mifugo katika kuimarisha afya za watoto chini ya miaka mitano ili kuondoa utapiamlo.

Rai hiyo ilitolewa na muuguzi msaidizi wa zahanati ya Nyakagoyagoye, Winston Byaton, wakati akielezea Nipashe jinsi hali ya utapiamlo kwa watoto wanaofika kwenye zahanati hiyo.

Byaton alisema, kwa kipindi cha Februari mwaka huu zahanati ilifanya vipimo kwa watoto 15 waliohudhuria na kubaini kati yao mmoja kuwa na utapiamlo mkali na wawili kuwa na wa kadri.

"Vipimo vyetu vilibaini watoto watatu kati yao 15 ndio walipata utapiamlo na hao ni kwa bahati walifika zahanati kupima... hapa ukienda vijiji utakuwa wapo wengi, lakini juhudi zetu ni kuwapatia elimu kwani vyakula wanavyo," alisema Byaton.

Alisema, ndani ya vijiji hivyo shughuli za wananchi ni kilimo na ufugaji licha ya wao kupenda kuuza badala ya kutumia kwenye familia zao kama chakula.

Paulina Gervas, mkazi wa Kijiji cha Nyamieli, alisema, tatizo la kuwa na watoto wenye udumavu ni kukosa elimu ya kuandaa chakula cha kumlisha.

"Wananchi wa kijiji hapa hufanya kilimo na mifugo na kuzalisha kwa wingi, shida ni nini? Kitumie kama lishe ya mtoto mdogo na muda gani atakuwa kupewa kwa siku," alisema Gervas.

Joel Mbaga mkazi wa Kijiji cha Nyakagoyagoye, alisema njia ya kusaidia ni vikao vya lishe kupitia mikusanyiko ya wananchi vijijini na kujua nini cha kufanya.Mbaga alisema, mtoto anadhoofika akiwa mdogo na ukikuta anacheza na wengine huwezi kujua kama ana miaka mitano, hana tofauti na wa miaka miwili.

## Vigwaza yalia uhaba shule za sekondari

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZA

DIWANI wa Kata ya Vigwaza Halmashauri ya Chalinze wilaya ya Bagamoyo, Mussa Gama, amesema kata yake kwa sasa inakabiliana na tatizo la uhaba wa shule za sekondari.

Amesema hali hiyo inasababisha baadhi ya wanafunzi kulazimika kutembea umbali mrefu.

Gama alisema wana uhitaji wa shule za sekondari tano ili kuwawezesha wanafunzi kufika shuleni kwa muda mfupi na kurejea nyumbani kwo.

Diwani huyo aliyaeleza hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ambapo alisema, vijiji kumi vilivyopo katika kata hiyo wanafunzi wanasafiri umbali mrefu hadi Vigwaza ilipo shule, jambo ambalo linasababisba baadhi yao kukatisha masomo kwa kutomudu umbali huo.

Gama alitaja maeneo ambayo wanafunzi wanatoka na kwenda hadi shule ya Sekondari ya Vigwaza kuwa ni Ruvu Darajani, Vigwaza Kambini, Vigwaza kwa Zoka, Milo, Kidogozero, Buyuni, Chamakweza, Mnindi, Kitonga na Visezi.

Alisema kwa sasa baada ya kupata eneo katika Kijiji cha Ruvu Darajani kutoka Ranchi ya Taifa ya Narco, wanatarajia kujenga shule ya sekondari itakayosaidia wanafunzi wa maeneo hayo kusoma karibu.

Aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwapatia eneo hilo ambalo watajenga mradi wa shule kushirikisha wananchi na Serikali.

Diwani huyo amewaomba wakazi wa Vigwaza kuendeleza umoja, upendo na mshikamano waliokuwa nao kwa miaka mingi, kuhakikisha wanajitokeza kwenye mikutano katika vijiji vyao ili waibue kero zinazowakabili zifanyiwe kazi kwa haraka.

**kwa sasa baada ya kupata eneo katika Kijiji cha Ruvu Darajani kutoka Ranchi ya Taifa ya Narco, wanatarajia kujenga shule ya sekondari itakayosaidia wanafunzi wa maeneo hayo kusoma karibu.**

# Bil. 1.5/- kuweka mfumo wa majitaka chuo kikuu

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI imeihakikishia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) itatoa Sh. bilioni 1.5 kukamilisha mfumo wa kudumu wa majitaka eneo jipya la Chuo Kikuu Mzumbe mkoani Morogoro kwa ajili ya kukidhi matumizi ya muda mrefu.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo,alipozungumza na kwa njia ya simu na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, ilipotembelea Chuo hicho kwa ajili ya kuangalia na kukagua mradi mkubwa wa ujenzi wa mabweni mapya manne yaliyojengwa kwa fedha zilizotolewa na Serikali kuu ambayo kwa sasa yamekamilika.

Mradi wa ujenzi wa mabweni manne ya ghorofa za kisasa ambayo yamejegwa kwa gharama ya Sh bilioni 6. 5 yana uwezo wa kuchukua idadi ya wanafunzi 1,024.

Mwenyekiti wa kamati hiyo baada ya kuzungumza na Katibu mkuu wa wizara hiyo Dk. Akwilapo, aliwaeleza wajumbe wa kamati hiyo kuwa wizara imeahidi kutoa Sh. bilioni 1.5 ifikapo Aprili mwaka huu za kujenga mfumo wa kudumu wa maji taka .

Kwa sasa licha ya kukamilika kwa ujenzi wa mabweni hayo, lakini mfumo uliopo wa majitaka uliojengwa hauna uwezo wa kukidhi mahitaji yaliyopo kwa miaka mingi ijayo .

Kuhusu uboreshaji wa elimu, aliushauri uongozi wa Chuo hicho kuona haja ya kuangalia upya mitaala inayofundishwa na kuandaa ile ambayo itawawezesha wahitimu kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea zaidi ajira za kuajiriwa.

Alisema Serikali inawekeza kwenye vyuo ikiwemo na Chuo hicho, hivyo ni matarajio ni kuona kwamba uwekezaji huo mkubwa unaleta matokea mazuri kwa wahitimu kwa kuitumia kujiajiri wao wenyewe badala ya kuendelea kutegemea ajira za kuajiriwa.

Naye Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Ganka Nyamsongoro, alisema licha ya kuwasilisha ombi ya fedha wizarani za ujenzi wa mfumo kudumu wa maji taka ,kwa sasa majengo mapya ya hosteli yanasubiri vifaa vitanda ili yaanze kutumika.

" Haya majengo tayari yana mfumo wa muda wa maji taka na jitihada zinazofanyika ni kuupanua zaidi mfumo huo na kuuingiza kwenye mfumo mkubwa wa majitaka kutokana na matarajio ya ongezeko la watu na majengo zaidi kwa baadaye," alifafanua Prof. Nyamsongoro mbele ya wajumbe wa Kamati hiyo.

Alisema Chuo pia kimepanga kunaza kununua samani zinazohitajika kwa kutumika fedha za mapato ya ndani wakati wakisubiri kupatiwa fedha kutoka Serikali kuu.

Akizungumzia kuhusu uboreshaji wa mitaala ya kufundishia, Mwenyekiti wa Baaraza la Chuo hicho, Prof. Mathew Luhanga, alisema kinachopaswa kufanyika kuboresha mitala inayotolewa kuendana na mazingira yaliyopo ili kuwezesha wahitimu kuwa na uwezo wa kujiajiri baada ya kuhitumu masomo yao.

Alisema ili kwenda na wakati na mahitaji halisi ya Ulimwengu wa wasasa, ni vyema Menejimenti za Vyuo Vikuu kikiwemo na Mzumbe kutoa fursa kwa wahadhiri wao kwenda kuhudhuria kozi fupi fupi kulingana na mabadiliko yanayojitokeza ili kuwajengea umahiri zaidi kulingana na mahitaji ya karne ya sasa.



Wanafunzi wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Semkiwa, Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, wakikalia meza na viti vilivyotolewa msaada na Benki ya NMB ikiwa ni sehemu ya benki hiyo kurejesha faida kwa jamii. Aliyesimama ni Mkuu wa Shule hiyo, Deborah Singu. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Rorya yamkumbuka JPM kwa miradi

**Na Samson Chacha, RORYA**

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Rorwa mkoani Mara, imetoa pole kwa familia na Watanzania kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Katika kikao hicho kilichofanyika mjini Utegi, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya

Rorya, Charles Ochele, alitoa pole kwa Watanzania na familia ya

Hayati Magufuli, na kuahidi kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuyaendeleza mazuri aliyoyaanzisha kwa taifa. Alisema msiba ni mkubwa kwa taifa.

Ochele alisema taifa limepata pigo kubwa kuondokewa na kiongozi shupavu na mtetezi wa wanyonge, hivyo wananchi wa Rorya tunatoa pole kwa

familia ya marehemu hususan Mama Janeth Magufuli na kwa Watanzania wote ili

kumwenzi kiongozi huyo.

"Tunatakiwa kumuunga mkono kwa nguvu zote kwa hali

na mali mama wetu Rais Samia ili tuweze

kuyaenzi matendo mema aliyotuachia ikiwamo miradi ya maendeleo kama kutujengea Hospitali ya Mkoa ya Kwangwa Mkoa wa Mara, Mahakama Kuu Musoma, Hospitali ya Wilaya Rorya na vituo vya afya... tushikamane tuwe kitu kimoja kumuunga mama yetu Samia, " alisema Ochele.

# Wakuu wa shule waguswa NMB kuwawezesha

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya walimu wakuu katika shule za sekondari na msingi Kanda ya Kaskazini wameeleza kuvutiwa na utaratibu wa misaada wanaopata kutoka Benki ya NMB, kwa kuwa imekuwa na mguso mkubwa kwenye maendeleo ya elimu nchini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti walimu hao kutoka mkoa wa Tanga, Kilimanjaro na Arusha wameeleza namna misaada kutoka NMB ilivyofika kwa wakati na kuwa sehemu ya mabadiliko kwenye kujifunza na kuwasaidia wazazi jukumu la kupatikana madawati, madarasa na vifaa vya kufundishia.

Ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa kurudisha kwa jamii asilimia moja ya faida inayopatikana kwa mwaka wa fedha, NMB wamekuwa na mfuko maalum ambao husaidia elimu, majanga na huduma za afya ambapo baada ya kukabidhi vifaa hivyo timu maalum huzunguka kuangalia ikiwa walengwa wamefikiwa na misaada husika.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Msambiazi wilayani Korogwe Mkoa wa Tanga, Selemani Kombo, alisema shule yake ufaulu umeongezeka baada ya kupata msaada wa kumalizia darasa na ofisi ya walimu.

"Mngekuja miezi kadhaa kabla ya leo (Machi, 2021) mngeshuhudia maajabu sana, maana kwa kweli shule hii ilikuwa na hali mbaya kwa upande wa ofisi ya walimu, hata baadhi ya madarasa hayakuwa hivi mnavyoyaona," alisema Mwalimu Kombo na kuongeza:

"Tulikuwa na kikao cha wazazi na viongozi wa shule, ndipo tulipopata taarifa kuwa Benki ya NMB inatoa misaada ya vifaa vya kuezekea na madawati, tukasema sisi shida yetu ni vifaa vya kuezekea. Asanteni sana tulipokea mabati na mbao za kuezekea, tunashukuru fedha ambazo tulipanga kuzitumia kuezeka tulizielekeza kwenye kupaka rangi na vifaa vingine hadi jengo likakamilika."

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Semkiwa iliyopo Korogwe, Deborah Singu, akizungumzia msaada wa viti 55 na meza zake, alisema msaada huo umewaonyesha namna wanafunzi wao walivyokuwa na kiu ya kukaa sehemu nzuri.

"Kwanza niwahakikishie msaada tumeupokea kama tulivyoomba, kimsingi hivi viti na meza ni imara sana hata wanafunzi wanavigombania. Cha kufurahisha hawa wanafunzi wa kidato cha nne baada ya kuona darasa lao ni zuri waliamua kuchangishana wakanunua saa ya ukutani ili wawe wa kipekee," alisema Mwalimu Singu.

Naye Mwalimu wa Taaluma shuleni hapo, Mwalimu Bashir Abdu, alisema kwa kiasi kikubwa shule yao ya Sekondari Semkiwa imekuwa na mabadiliko makubwa kitaaluma baada ya wanafunzi kupata nafasi nzuri za kukaa madarasani.


Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 30, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





Ukurasa 13

Sekondari aina yake kwa ajili ya wenye ulemavu tangu uhuru




Ukurasa 14

**Biashara mtandaoni inavyoteka mfumo matangazo ya soko kwa gharama nafuu**

NA BEATRICE PHILEMON

# MAZITO YA VIJANA ELIMU KILWA NJINJO

## • Waonyesha maajabu ujenzi madarasa • Baada kuelimishwa, wameamka vilivyo • Kilichoshindikana, wao wamekiweza • TAMISEMI, Halmashauri zawaunga mkono • Mpya sasa washinikiza watoto wafugaji wakasome

MTU anapozungumzia kijiji cha Njinjo, huenda si wote wana ufahamu. Kipo katika kata ya Njinjo umbali wa kilomita 69, kutoka ilipo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi. Kuna mambo yametokea ya mapinduzi makubwa katika elimu.

Hapo ni mahali ambako ni umbali wa kilomita mbili na nusu, kuna shule na kijiji baada ya kuhama pa awali kutokana na mwanzo kuathiriwa na mafuriko ya bahari.

Nini kinaendelea? Ni namna zao la mafunzo ya uongozi, ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali za umma, ikiwamo ulipaji kodi ulivyoleta mwamko kwa vijana kushiriki na kusimamia miradi ya ujenzi wa shule, sambamba na mingine ya maendeleo mahali hapo.

Asilimia kubwa ya wakazi, wakiwamo vijana wa kijiji hapo, ni wakulima wanaotegemea sana shughuli ya kilimo cha mazao ya biashara, ufuta na korosho. Pia kuna chakula; mahindi, mpunga, mtama na muhogo.



Vijana wakipata mafunzo ya uongozi, ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali za umma na ulipaji kodi katika kijiji cha Njinjo, yaliyotolewa na Shirika la ActionAid Tanzania, Kanda ya Kilwa. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

### MWAMKO WAO

Madadi Mkape, Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Kata ya Njinjo (KIYODI), ameiambia Nipashe kuwa baada ya kupata mafunzo ya ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali za umma, uongozi na ulipaji kodi, hivi sasa hali imebadilika.

Anasema, vijana wengi wameamka na wahudhuriaji wa mikutano mbalimbali ya kijiji, wanasimamia miradi yake, ikiwamo ujenzi wa madarasa na miradi mingine.

Mkape anaishukuru Asasi ya ActionAid Kilwa, kwa kuwapa vijana mafunzo, kwani nyenzo iliyowafumbua macho asilimia 75 ya idadi yao.

Hivi sasa wamekuwa wahudhuria mikutano ya vijiji, pia ya dharura wakiwa na weledi wa kuhoji kilichomo kwenye ajenda jambo lililo tofauti sana na miaka ya nyuma.

"Kwa mfano, baada ya kupata mafunzo, tuliibua changamoto ya ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Njinjo," anaeleza.

Katika ufafanuzi wake, Mkape anasema awali Halmashauri ya Kijiji cha Njinjo, ilianza kujenga madarasa mawili na walikuwa wamefikia hatua ya ujenzi wa 'rinta' ikaonekana wametumia shilingi milioni 18.

### WAINGILIA KATI DOSARI

"Mimi kama Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Kata ya Njinjo, sikupendezwa na ile takwimu ya hela iliyotumika. Niliona kama tunafanyiwa isivyo, kwa sababu mbali na hiyo hela, pia kuna wafadhili walichangia mifuko 145 kusaidia ujenzi," anasema.

Anasema, kati ya mifuko 145, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Vedasto Ng'ombale Mwiru, alichangia mifuko 70 na Mangungu Ali, alichangia mifuko 75, iliyotolewa mwaka jana.

Kijana huyo anasema baada ya kuona walakini huo, anaeleza hatua yake kwamba: "Nilimwomba Mwenyekiti wa Kijiji aitishe Mkutano Mkuu wa Kijiji, ili watueleze zile hela zimetumika vipi.

"Pia katika mkutano huo, niliomba vijana wafike kwa wingi, ili tutakaposomewa mapato na matumizi, tujue hiki kilitumika vipi, lakini bahati mbaya huo mkutano haukufanyika.

"Ila baadaye sisi kama vijana tuliomba tena kamati iliyosimamia ujenzi kwa mara ya kwanza na kamati iliyopo kwenye ujenzi waingie vijana. Kwa bahati nzuri, walikubali na tukaingia vijana 11," anasema na kuendelea: "Kati ya hao, wavulana tisa, wanawake wawili na tumeweza kusimamia ujenzi wa madarasa matatu."

Anasema, pia Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kupitia ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, iliridhishwa na hatua iliyochukuliwa na kuwapatia fedha shilingi milioni 30, ili kumalizia ujenzi, kutoka pale serikali ya kijiji ilipokuwa imeishia na tundu tano za choo.

Kiongozi huyo wa kijana anasema, ujenzi wa madarasa matatu umeshakamilika, huku akiwa na ufafanuzi wa ziada: Pia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imetoa tena shilingi milioni 62.5, katika Shule ya Msingi Njinjo ili kujenga madarasa matano.

### WANAVYOFANYA KAZI

Mkape anasema, wao jukumu lao haliishii katika usimamizi

INAENDELEA UK.12

# MAZITO YA VIJANA ELIMU KILWA NJINJO

INATOKA UK.11

pekee, bali wanawajibika kwa vitendo kuhakikisha vinavyotakiwa katika shughuli ya ujenzi vinafika kwa wakati, ikiwamo mchanga, kokoto, tofali na vifaa vingine.

"Kabla ya vijana kuingia kwenye kamati, ilikuwa kama 'shamba la bibi' kijiji cha Njinjo. Kwa hiyo, mtu anaamua anavyotaka yeye anakula, halafu mwisho wa picha inaonekana kwamba hakuna kitu chochote kinachoendelea," anasema.

Katika ufafanuzi wake wa hoja hiyo, Mkape anasema tangu wao vijana waingie katika uamuzi ndani ya kamati husika, hivi sasa msamiati 'shamba la bibi' linatoweka, pesa zote za serikali au rasilimali za umma, zinatumika kwa usahihi.

"Kama ikitokea imetengwa milioni tano itumike sehemu fulani, basi inatumika kama ilivyokusudiwa," anasisitiza.

### WITO KWA VIJANA

Mkape anasema, vijana wanapaswa kuhudhuria mikutano ambayo ndiyo inapanga kila kitu na anawataka vijana wasikose kuhudhuria mikutano, kwani kinyume chake ni kujiacha nyuma katika linalohusu maendeleo yao.

"Mimi kama Mwenyekiti, niwaombe vijana twendeni kwenye mikutano, lakini twendeni kwenye mkutano siyo kukaa tu," anasema.

"Tunahoji mapato na matumizi, kipi kimekusanywa, kipi kimetumika, kipi kilichobaki na je, yale yote tuliyoazimia kwenye mkutano mkuu yametekelezwa au kipi kimetekelezwa?" Anahoji.

"Vijana wana wajibu wa kufanya hivyo, kwa sababu wanaoathirika zaidi siyo wazee ni sisi vijana. Kwa hiyo, ni vizuri kushiriki katika mikutano mbalimbali ya vijiji, kwa ajili ya maendeleo ya vijiji vyao na maisha yao kwa ujumla," anasema.

### KIKWAZO KIKUU ELIMU

"Katika suala la elimu, asilimia 75 ya vijana katika kata ya Njinjo wanapenda sana kusoma, wengi wanajua umuhimu wa elimu na mzazi kama mzazi wa kabila la Wangindo, hawawezi kukubali mtoto wake bila kwenda shule," anasema Mkape.

### SHIDA YA WAFUGAJI

Hata hivyo, Mkape anatoa angalizo la kasoro katika amabalo katika Kata ya Njinjo, hali bado haipo sahihi, watoto wengi kutoka jamii ya wafugaji katika kitongoji cha Mchemela A, hawaendi shule.

Kwa mujibu wa Mkape, kundi kubwa la jamii ya wafugaji na hasa wanaotoka mikoa ya mbali, ikiwamo mikoa ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa, kati ya mwaka 2013 hadi 2014, waliingia kijijini Njinjo na kufanya makazi.

"Hivi sasa ukipita kwenye kambi zao, kuna watoto wengi, lakini hawapelekwi shuleni," anasema Mkape na kuongeza kwamba kuna wimbi la vijana na watoto waliopo mitaani na hawaendi shule.

Mkape anawanukuu vijana na watoto hao kutoka jamii ya wafugaji wanachosema kwamba "mtu anapofikia umri wa kwenda shule, anafahamishwa kifamilia kwamba, utajiri wake hauko shuleni."

Kijana huyo anasema binafsi akiwa Mwenyekiti Kata ya Njinjo amejitahidi kuwashirikisha na kuwaita wazazi kwenye kikao kuhusu elimu na majibu anayopewa "utajiri nimeshaupata, elimu ya nini sasa?" anasema Mkape.

"Baada ya hapo niliamua kwenda kuripoti kwa (Ofisa) Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kata aliwaita wazazi na kuwatolea ukali kuhusu hii hoja. Toka hapo, baadhi ya wazazi wameanza kupeleka shule mtoto mmoja mmoja, lakini hailingani na watoto waliobaki nyumbani.

"Mimi ninachoona, kwanza tuanze kuelimisha wazazi kuhusu umuhimu wa elimu, kwa sababu hata wazazi wenyewe wengi hawajui kusoma. Ukishamshibisha mzazi, atakuwa ameelimika, atajua umuhimu wa elimu na hatimaye kupeleka mtoto wake shuleni," anasema.

Kiongozi huyo wa vijana anasema, binafsi alifanya utafiti katika kitongoji hicho chenye ufugaji na kugundua kuwa sehemu kubwa ya wazazi hawawezi kusoma hata meseji za simu zao, ukiwa udhihirisho kwamba hawajui umuhimu wa elimu.

### MWALIMU MKUU NJINJO

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Njinjo, Constantine Mjungu, ana ufafanuzi wake kuhusu shule yake: "Hadi sasa ujenzi umeishakamilika, kati ya madarasa hayo, darasa moja litatumika kama ofisi ya Mwalimu Mkuu na yaliyobaki yatatumiwa na wanafunzi," anasema.

Shule ya Msingi Njinjo ilianzishwa mwaka 1945 na mpaka sasa, ina jumla ya walimu wanane na wanafunzi 824, matundu matatu ya choo yaliyozungushiwa mabati, ikiwa na lengo la kuwa na madarasa manane, kati yao matano yanaendelea kujengwa.

Hadi sasa, anasema bado wanahitaji nyumba nane za walimu, matundu 36 za choo kwa ajili ya wanafunzi, matundu manne kwa ajili ya walimu, kwa sababu hadi sasa walimu hawana choo cha kujisitiri.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu, hali ya vyoo vilivyopo sasa, wanaenda kujissitiri jirani na hiraji lao la haraka ni kupatiwa madarasa matatu kwa ajili ya wanafunzi.

# MASHAIRI YA KUENZI NA PONGEZI

## UMEJENGA, UMEJENGA JOHN POMBE MAGUFULI

1. Umejenga umejenga,
Umejenga umejenga,
Sifa zako za kujenga,
John Pombe Magufuli.

2. Dodoma umeijenga,
Dasalamu umejenga,
Nchi yote umejenga,
John Pombe Magufuli.

3. Kote kote ni kujenga,
Hakuna anayepinga,
Ustawi ulilenga,
John Pombe Magufuli.

4. Barabara alijenga,
Na masoko amejenga,
Viwanja ndege kajenga,
John Pombe Magufuli.

5. Job Ndugai katunga,
Maneno vema kapanga,
Haya yote yakulenga,
John Pombe Magufuli.

6. Kazi watu wamefunga,
Njia zote mejipanga,
Hiki chote ni kipenga,
John Pombe Magufuli.

7. Da Tulia kajipanga,
Hotuba aloitunga,
Biblia kukulenga,
John Pombe Magufuli.

8. Hatuwezi kuipinga,
Mambo Mungu amepanga,
Ndivyo alivyojitenga,
John Pombe Magufuli.

9. Mengi aliyoyapanga,
Ya Dodoma kuijenga,
Kumbukumbu ni kujenga,
Pasi na ya kufeli.

10. Bomba la maji kujenga,
Toka ziwani lilenga,
Eapoti kuijenga,
Msalato ni mahali.

11. Maisha yake kujenga,
Ndiyo hasa alijenga,
Lijenga bila kuringa,
John Pombe Magufuli.

**Lwaga Mwambande,
Dar es Salaam**

## MAGUFULI HUFI KAMWE - RAIS NYUSI

1. Mwenye moyo kama wako, Magufuli hafi kamwe,
Huo ni ujumbe wako, Magufuli hufi kamwe,
Ni hayo matendo yako,
yakufanya hufi kamwe,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

2. Kama wasikia huko,
jua kwamba hufi kamwe,
Sababu ni mambo yako,
yanafanya hufi kamwe,
Huo uongozi wako, wanasema hufi kamwe,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

3. Na Cyril Ramaphosa,
na yeye kakusifia,
Kiongozi wa kisasa, alivyokufurahia,
Ukarimu wako hasa, vile ulimfanyia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

4. Ulivyoenda Sauzi,
alivyoapishwa pia,
Akumbuka wazi wazi,
heshima limfanyia,
Vile anajua wazi, safari lizuia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

5. Ametoa shukurani,
kwa nchi ya Tanzania,
Afrika ya Kusini, ubaguzi kuishia,
Kwamba ni hapa nchini,
harakati lianzia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

6. Ulitaka watu wote,
Afrika na dunia,
Kiswahili kiwe kote,
waweze kukitumia,
Kama kumvika pete, shuleni wajifunzia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

7. Matatu katutajia,
Magufuli msifia,
Rushwa kutoiachia,
ishamiri Tanzania,
Viongozi kuusia, umimi kututumia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

8. Vile lisisitizia, uchumi wa Tanzania,
Na kanda ikifikia, maendeleo ya nia,
Mwanamajumui pia, ndivyo tulikusikia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

9. Rais wa Botswana,
Masisi kamsifia,
Ya kwamba wanafanana,
na Nyerere kuvutia,
Uongozi wa maana, kwa kanda na Tanzania,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

10. Botswana kama Sauzi, uamuzi mefikia,
Kiswahili wazi wazi, mitaala yatimia,
Wanamuenzi kwa wazi,
baba aliyeishia,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

11. Na kwake Mama Samia, ujumbe amesikia.
Walivyosisitizia, mkono mshikilia,
Kazi akijifanyia, kuijenga Tanzania,
Rais wa Msumbiji, ndivyo anakuambia.

**Lwaga Mwambande,
Dar es Salaam**

## RAIS WETU MAMA UNAWEZA

1. Aliyesimama hapa,
Rais wa Jamhuri,
Amesema hapa hapa,
Tomaso pata habari,
Atuaminisha hapa, kazi yake tusubiri,
Mama Samia Suluhu,
Mungu atakuwezesha.

2. Maisha yako ni chapa,
wewe hasa ni mahiri,
Historia yalipa, kwa kweli umesafiri,
Hadi unafika hapa, kwa kweli uko ngangari,
Mama Samia Suluhu,
Mungu atakuwezesha.

3. Kazi huko hukukwepa,
likabili kwa hadhari,
Uliivunja mifupa, mingi kwenye uwaziri,
Umakamu hukukwepa,
wengine wanasubiri,
Mama Samia Suluhu,
Mungu atakuwezesha.

4. Bunge Katiba ni chapa,
uliuweka mhuri,
Wajumbe ulivyowapa,
kujadili kwa uzuri,
Wengine tulio hapa, tulikujua uzuri,
Mama Samia Suluhu,
Mungu atakuwezesha.

5. Mwanamke unalipa,
hebu ongoza safari,
Nchi izidi kusepa, amani na utajiri,
Hakuna la kuogopa, Tanzania nchi nzuri,
Mama Samia Suluhu,
Mungu atakuwezesha.

6. Viongozi wote hapa,
uwanja wa Jamhuri,
Mkono wameshakupa,
ukizikuta hadhari,
Wala hawajaongopa,
mtaenenda vizuri,
Mama Samia Suluhu,
Mungu atakuwezesha.

**Lwaga Mwambande,
Dar es Salaam.**

ELIMU

NA AUGUSTA NJOJI, ARUSHA

# Sekondari aina yake kwa ajili ya wenye ulemavu tangu uhuru

• Jafo: Elimu bure yawaibua waliofichwa nyumbani



Wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule Maalum ya Sekondari Patandi, wakiwa katika mjumuiko wao. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

WATOTO wenye ulemavu ni kundi maalum linalohitaji kupewa mahitaji sawa na wengine, ili kufikia ndoto zao.

Kundi hilo linajumuisha wenye ulemavu mbalimbali wa viungo vya mwili, ikiwamo miguu, mikono, macho na masikio.

Kutokana na azma ya serikali kuhakikisha hakuna mtoto anayeachwa nyuma kwenye utoaji elimu, ilianza mikakati yake kwa ajili ya watoto, kwa kujenga shule maalum ya Sekondari ya Patandi, iliyoko mkoani Arusha.

Ni shule kwanza kujengwa nchini kwa ajili ya watoto wa kada hiyo na ina uwezo wa kuchukua watoto takriban 600, kati yao wanaoishi bwenini wako 416.

Hivi karibuni Nipashe ilitembelea shule hiyo iliyoanza kupokea wanafunzi, baada ya serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), kukamilisha ujenzi wake kupitia mradi uitwao 'Lipa Kulingana na Matokeo' au (EP4R) na ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 3.6.

**MKUU WA SHULE**

Mkuu wa Shule hiyo, Janeth Mollel, anasema hadi sasa kuna jumla ya wanafunzi 143, ambao kati yao 93 ni wenye ulemavu ambao wamesharipoti kuanza masomo yao, wiki kadhaa zilizopita.

"Hii shule inachukua watoto hawa wenye mahitaji maalum nchi nzima, tunashukuru serikali chini ya Rais John Magufuli (zama za uhai wake) kwa kuona umuhimu wa kujenga shule hii, ambayo ni ya kipekee Tanzania nzima na inawezekana pia Afrika Mashariki," anasema.

Mwalumu Mollel anasema, shule hiyo upekee wake inachukua wanafunzi wa aina zote. Anafafanua: "Kuna watoto wenye ulemavu wa aina zote wanasoma hapa, watoto wasiosikia na wanaotumia viti mwendo.

"Miundombinu ya shule hii imezingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu, kuna vyumba maalum kwa ajili ya wanafunzi ambao wana ulemavu mkubwa wa viungo, ambapo vyumba hivyo vina vyoo ndani."

Anasema walimu wao ni waliosomea kufundisha watoto wa aina hiyo na wanafunzi wasio na mahitaji maalum ili kushirikana nao na kujiona hawajatengwa na jamii.

"Wanakula na kucheza na walimu, kwa ujumla watoto wanafurahia maisha ya hapa Patandi," anasema.

"Serikali imeona umuhimu wa kuwa na shule hii na wanasoma bure wao na kulala bure, hii ni shule ya mfano," anatamka, huku akitoa rai kwa jamii kuacha kuwaficha watoto hao ili wasome na kufikia ndoto zao.

Mwalimu Mkuu anaiomba serikali kujenga shule nyingine ya mfano za aina hiyo kwenye maeneo mengine, ili wanafunzi waondokane na kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

"Kwa mfano, nina mtoto anaitwa Rebeca anatokea Kusulu Kigoma, sasa ili kuondokana na tatizo la kusafiri umbali mrefu, ni vizuri ikaona umuhimu wa kujenga shule kama hii kwenye maeneo hayo," anasema.

**WANAFUNZI WANENA**

Mmoja wa wanafunzi hao, Nurueli Thomas, anasema, mazingira ya shule hiyo yanaendana na hali halisi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Tunashukuru serikali kwa kujenga miundombinu hii mizuri na ya kuvutia, walimu wanafundisha vizuri, miundombinu hii itasaidia kusoma vizuri na kufikia ndoto zetu, tunaahidi serikali hatutaiangusha tutafaulu vizuri kwenye mtihani wa kidato cha nne," anasema.

**N/ KATIBU MKUU TAMISEM**

Akizungumzia kuhusu shule hiyo, Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Gerald Mweli, anasema shule hiyo ina miundombinu bora na saidizi kwa watoto wenye mahitaji maalum, pia walimu 11 hadi sasa wameshapelekwa na serikali kufundisha watoto hao na hakujawahi kuwapo shule aina hiyo tangu uhuru wa nchi.

"Hatujawahi kuwa na shule maalum kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum kwa sekondari, kuna utofauti kwenye njia za kupita zinamwezesha mtoto mwenye ulemavu kupita, mabweni yametengenezwa kitofauti," anasema.

Anaongeza: "Shule ya Patandi imejengwa kwenye chuo ambacho serikali imekianzisha kwa ajili ya kufundisha walimu watakaofundisha watoto wenye mahitaji maalum na imejengwa kupitia Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R)."

Naibu Katibu huyo, anasema lengo la kujenga shule hiyo ni watoto hao watakapofaulu waendelee na elimu ya sekondari.

"Awali walishindwa wengine kuendelea na shule, kutokana na kutokuwa na miundombinu rafiki. Tumeweka sera ya elimu jumuishi ili watoto wasio na changamoto wawasaidie wenye uhitaji," anasema.

"Serikali imejipanga kupokea watoto hawa, tusiwafiche na tuwalinde ili wapate elimu," anaogeza.

Pia, Mweli anazungumzia uandikishaji wa watoto hao kwenye shule za msingi nchini, anasema kumekuwapo ongezeko la watoto wenye mahitaji maalum wanaoandikishwa kwenye shule hizo kwa miaka mitano sasa.

Anasema, hadi sasa kuna zaidi ya watoto wa aina hiyo 54,000 walioandikishwa shuleni na ongezeko hilo limetokana na Mpango wa Elimu Bila Malipo, pia mwamko wa wazazi kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu.

Mweli anasema, kutokana na ongezeko hilo serikali, ilianza kutoa mafunzo kwa walimu takribani 60,000 wa elimu ya awali na msingi, ili wawahudumie watoto hao watakaokuwapo kwenye shule husika.

"Sisi tunataka shule zetu hizi za kawaida pamoja na kwamba sio za watu wenye mahitaji maalum, lakini shule zingine zimeimarisha miundombinu yake, ili kutoa huduma kwa watoto na tumenunua vifaa vya kutosha," anasema.

**WAZIRI JAFO**

Waziri Ofisi ya Rais mwenye dhamana na TAMISEMO, anasema serikali imetoa kipaumbele kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupata elimu katika mazingira rafiki kwao na imekuwa ikiwanunulia na kuwawezesha vifaa vya kujifunzia na kufundishia elimu maalum.

Jafo anasema, kwa kipindi cha miaka mitano ya sasa serikalini kuna ongezeko la shule kwa ajili ya wanafunzi wa mahitaji maalum kwa asilimia 46.1 kwa shule za awali, asilimia 23.9 kwa shule za msingi na asilimia 24.6 kwa shule za sekondari.

Anasema kwa upande wa uandikishaji wanafunzi, umeongezeka kwa asilimia 46.1 kwa shule za awali, asilimia 34 kwa shule za msingi na asilimia 74.6 kwa shule za sekondari. Waziri huyo anasema, katika kipindi hicho pia walimu wataalamu wa elimu hiyo maalum 418 waliajiriwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, kwa shule za msingi na sekondari.

Jafo anasema katika kipindi hicho mabweni 289 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji hayo yamejengwa na yanatumika, huku mengine 32 yanaendelea kukamilishwa.

Anabainisha kwamba, katika kipindi hicho pia kuna fedha Sh. bilioni 42.3 zimetumika kwa ajili ya chakula katika shule za msingi za bweni zinazohudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Pia anasema idadi ya wanafunzi wanaofaulu mitihani ya darasa la saba kwenda sekondari imekuwa ikiongezeka kutoka wanafunzi 1,117 ambayo ni asilimia 69.9 kwa mwaka 2016 hadi kufikia wanafunzi 2,534 ambao ni asilimia 76.3 kwa mwaka 2020.

TEKNOLOJIA

NA FRANCIS MATHAYO

# Biashara mtandaoni inavyoteka mfumo matangazo ya soko kwa gharama nafuu

BIASHARA ya mtandaoni au maarufu 'digital business' ina maana gani? Kimsingi, ni aina inayohusisha kubadilishana taarifa za biashara kupitia mitandao ya mawasiliano.

Ni aina ya teknolojia iliyopo sasa na imebadili mfumo wa biashara wa awali uliowahitaji muuzaji na mnunuzi kuonana. Sasa ni mfumo wa biashara unaomruhusu muuzaji na mnunuzi kufanya biashara, wakiwa katika maeneo tofauti.

Teknolojia hiyo, pia imeongeza thamani ya biashara kwa kuzingatia kuwa imeweza kurahisisha shughuli za kila siku za biashara, kuongeza wigo wa masoko na kuongeza ufanisi wa kuhudumia kwa wateja.

Biashara ya mtandao wa mawasiliano, imekuwa ikikua kwa kasi kuanzia miaka ya 2000, kutokana na kuongezeka watumiaji wa mtandao huo wa taarifa ya mtandao wa (data report) hadi mwanzoni mwa mwaka huu Januari, inaainisha kwamba kulikuwapo watumiaji mtandao bilioni 4.66 duniani kote, hali inayoonyesha kulikuwapo ongezeko la watumiaji wa mtandao milioni 319 kwa mwaka jana.

Hiyo inatajwa kuwa sawa na ongezeko la asilimia saba, ikilinganisha na mwaka 2019. Nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania, zinaonyesha kuongoza kwa ongezeko kubwa la watumiaji mitandao.

Wastani wa utumiaji mtandao kidunia, unatajwa kuwa saa saba kwa kila mtumiaji kwa siku na taarifa za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), mwaka uliopita, zinaonyesha kuna jumla ya watumiaji mitandao milioni 27, Tanzania ikiwa na ongezeko la watumiaji zaidi ya milioni moja tangu mwaka 2019.


Aidha, watumiaji mitandao ya kijamii kwa mwaka jana walikuwa milioni 4.5 sawa na ongezeko la asilimia 13 duniani, kukiwapo watumiaji mitandao ya kijamii kiwango cha asilimia saba kitaifa.

### ONGEZEKO SOKONI

Lingine katika hilo, kuna suala la kuongezeka idadi ya watumiaji mitandao hiyo kwenye soko la mtandao, idadi kubwa ya watumiaji wanapata nafasi kupitia bidhaa mbalimbali zinazobandikwa na wafanyabiashara katika mitandao.

Soko la mtandaoni ni linalowakutanisha wanunuzi na wafanyabiashara katika mtandao, kupitia soko hilo, wateja wanaweza kununua bidhaa kutoka nje ya nchi au ndani na ya nchi na kufikishiwa bidhaa mpaka mlangoni.




Matangazo ya mtandaoni katika picha tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kuna watu wengi wamekuwa wakijiuliza ni biashara gani inaweza kufanyika na kupata masoko ya mtandaoni? Kuna wafanyabiashara wadogo wamekuwa wanadhani kwamba, masoko ya mtandao ni maalumu kwa wafanyabiashara wakubwa, hali inayotokana na kuhofia gharama zinazohusiana na matangazo ya mtandaoni.

Ukweli uliopo ni kwamba biashara yoyote inaweza fanyika mtandaoni, pasipo kujali kinachouzwa na ukubwa wake, ili mradi ina uhalali, ikiwa ni biashara zinazoweza kufanyika mtandaoni.

Hapo kuna orodha kama; uuzaji nguo, vinywaji, vyakula, vifaa vya ofisini na shuleni, thamani, vifaa vya ujenzi, matunda, mbogamboga, vyombo, vifaa vya umeme.

Pia mtandaoni kunaweza kukauzwa huduma kama zinazohusu matengezo ya magari, ujenzi, utengenezaji samani, uuzaji wa nyimbo na filamu, hali kadhalika huduma za usafirishaji.

### FAIDA ZAKE

Masoko ya mtandaoni yamekuwa na faida kubwa kwa wafanyabiashara na kuwa chachu ya kuendelea kwa biashara ndogo nyingi nchini, pia za kati.

Hilo linapatikana kwa kuongezeka idadi ya watumiaji mitandao ya kijamii, hali inayowapa motisha wafanyabiashara kuendelea kutangaza bidhaa kwa masoko ya mtandaoni.

Wengi wanatumia mitandao ya kijamii kutangaza bidhaa zao, wengine wanatumia tovuti na mengine yanayohusiana nayo kuwafikia wateja kokote waliko.

Kuna baadhi ya mitandao ya kijamii maarufu inayotumiwa na wafanyabiashara, inayoangukia katika makundi yanayojulikana kwa majina yake kitaalaamu kama: "Facebook; Instagram, Whatsapp; Telegram; Twitter na Youtube."

Biashara kubwa kama benki na mitandao ya simu, zinatumia mifumo ya mitandao ya kijamii kutambulisha bidhaa zao mpya, au kuwasiliana na wateja moja kwa moja na kwa haraka.

Vivyo hivyo, wafanyabiashara wadogo na kati wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii kutafuta masoko mapya ya bidhaa zao na kuwasiliana na wateja wao.

### WENGI WANAVYOGUSWA

Kuna Faida nyingi zinatajwa kwa mfanyabiashara anapoingia katika soko la mtandaoni, mojawapo ni uwezo wa kuwafikia wateja wengi ndani ya muda mfupi, kwa ujumla wao, ndani na nje ya nchi.

Inapozingatiwa kwamba watumiaji mtandao ni wengi, inakuwa sura pana kwa bidhaa za mfanyabiashara anayeuza katika soko la mtandao, kufikia wateja wengi ndani ya muda mfupi.

Uko mtazamo kwamba, mfanyabiashara anayetumia soko la mtandaoni, anakuwa na wigo mpana wa kuzitangaza bidhaa zake na unampa nafasi ya kuuza bidhaa zake nje ya eneo aliko.

Lingine, ni biashara ya mtandao unatoa nafasi ya kuchagua hadhira mtu unayoitaka kwa ajili ya biashara, pasipo kujali ama yuko ndani ya nchi au yuko nje, mathalani hivi sasa kuwapo wateja wengi wanaonunua bidhaa kutoka nchi za mbali kama vile China.

Hapo ndiko kuna njia za mtandao kama zilizotajwa awali za Instagramu au 'Facebook'. Katika hilo, kunaelezwa, mathalani mfanyabiashara wa nguo aliyeko Dar es Salaam, anaweza kubandika nguo anazouza katika ukurasa wake, kisha mteja aliyeko mkoa jirani wa Dodoma akanunua.

Katika gharama za kutafuta wateja, kunatajwa kuwapo nafuu maradufu mtandaoni, ikilinganishwa na njia mbadala zilizopo.

Mitandao kwa kiasi kubwa, inaelezwa hakuna gharama yoyote mfanyabiashara anayotozwa kwa kubandika (post) bidhaa zake, gharama inaweza kujitokeza tu pale anapohitaji tangazo lake liwafikie watumiaji wengi zaidi.

Ili kufanya malipo mteja na mununzi huwa kuna mifumo miwili, mfanyabiashara anaweza kutumiana katika kuwafikia wateja wengi zaidi.

Mosi, kuna suala la utumiaji matangazo yaliyodhaminiwa, inaanzia dola moja ya Marekani hadi mbili (Sh. 2,300 na Sh. 2,600) wakitumia watu mashuhuri na wenye wafuasi wengi kwenye mitandao ya kijamii na kwa ujumla, inatajwa kuwa bado ni nafuu, kwa sababu inawezesha kufikia watumiaji wastani kati ya 1000 hadi 5000.

Kwa kurejea mbadala wake, kufikisha ujumbe kwa kiasi hichi cha umma, mbadala wa kutumia vipeperushi, ingetumia kati ya Sh. 50,000 kwa vipeperushi 1000 wanazoweza kuvigawa kwa jamii.

Lingine la manufaa mtanadoni, anataja ni namna ujumbe unafikia kwa namna sahihi kwa walengwa, hata kuongeza maswali machache ya kutakiwa uelewa zaidi kutoka kwa wateja wake.

Inaelezwa, mara nyingi bidhaa za mtandao zimekuwa zikiwekewa maelezo ya kina yanayomtosheleza mteja kufiia uamuzi.

Katika mfumo huo wa mawasiiano ya nmatangazi mtandaoni, taasisi kuwa zina utamaduni wa kuweka majibu ya maswali yanayoulizwa kila mara, ili kupunguza ufinyu wa uelewa wa maswali mengi kutoka kwa wateja hivyo kuongeza wigo mpana wa kuhudumia wateja.

Yapo manufaa yanayotajwa kwamba mfanyabiashara anayewasiliana mtandaoni, ana fursa ya kunufaika zaidi, kutokana na kuwa na muda wa kutosha kuhudumia wateja wake, kwa sababu hafungwi na muda wa kufanya biashara na wateja wake.

Katika wakati huu ambao matumizi ya mitandao imekua ikiongezeka siku hadi siku, soko la mtandao ni halikwepeki kwa mfanyabiashara yeyote nchini.

Ujumla wake ni kwamba, asasi inayosaidia kuongeza kipato cha biashara, kukuza wigo wa huduma wateja wanaoongezwa, pia idadi yao thamani ya biashara, ni muhimu kwa wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa kuingia katika soko la mtandaoni.





# Askofu KKKT ataka Samia apewe ushirikiano

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, amewaomba viongozi na wananchi kumpa ushirikiano Rais mpya Samia Saluhu Hassan ili kufikia maendeleo yaliyokusudiwa.

Askofu Kinyunyu, alitoa kauli huyo wakati mahubiri yake kwenye ibada ya kuzindua ushariki mpya wa KKKT mwangaza uliopo jijini hapa mwisho wa wiki.

Aliwaomba viongozi wa serikali na wananchi kumpa ushirikiano Rais mpya Samia ili aweze kutekeleza majukumu yake mapya kwa nafasi hiyo na nchi ifikie malengo ya maendeleo yaliyokusudiwa katika kipindi cha miaka ijayo.

"Tunamshukuru Mungu ametuvusha salama katika kipindi kigumu cha majonzi ya kuondokewa na mpendwa wetu, Dk. John Magufuli aliyekuwa rais wetu, lakini Mungu huyo huyo ndiye aliyetupa huyu rais mpya mama yetu Samia kushika nafasi hiyo kwa hiyo watu wote tumpe ushirikiano," alisema.

Kadhalika, alisema Watanzania wengi hawana shaka naye kwa sababu amekuwa Makamu wa Rais kwa kipindi kirefu cha utawala Hayati Dk. Magufuli na mipango mingi iliyokusudiwa anaifahamu kinachohitajika ni kupewa ushirikiano.

Pia aliwataka viongozi wa dini zote kuendelea kumwombea Rais Samia ili Mungu ampe hekima ya kuongoza nchi na watu wake.

"Vingozi wa dini na waumini wetu tunawaomba kumwombea rais wetu ili Mungu ampe afya njema ili aweze kulionGoza taifa letu kwa amani," alisema.

Alimpongeza kwa kuweka historia ya kuwa rais wa kwanza mwanamke Afrika Mashariki na anaamini kuwa ataonyesha mfano kwa nchi zingine ili kuendelea kuwaamini kinamama katika madaraka ya juu serikalini.

Alisema kinamama wakipewa nafasi wanaweza kwa sababu katika familia wanajua maendeleo ya watu na vitu kwa sababu ya kuwa karibu na familia.

Kwa upande wake Mchungaji wa Usharika wa Mwangaza, Edda Mwambo, alilishukuru kanisa hilo kwa kuendelea kuwaamini wanawake kuwa wachungaji.

Mbwambo alisema katika kanisa hilo wanawake wengi wamepewa nafasi ya kwenda kusomea uchungaji na kuongoza makanisa hayo kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema idadi ya wanawake ni wengi katika jamii na kwamba wakipewa nafasi za uongozi watasaidia kuwahamasisha kuondoa mfumo dume uliozoeleka kwenye maeneo mengi duniani.

## 'Rais Samia aombewe kutekeleza yaliyoachwa na JPM'

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

MAKAMU Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino mkoani Dodoma, Keneth Yindi, amewaomba Watanzania kuelekeza nguvu zote za maombi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ili aweze kutekeleza na kuendeleza yote yaliyoachwa na Hayati Rais Dk. John Magufuli, kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Aliwaomba kumwombea kwa Mungu Rais Samia ili afanikishe kukamilisha maono yake ya miradi iliyokuwa imeshaanzishwa na mtangulizi wake itekelezwe kwa wakati.

Alisema Watanzania wana matumaini makubwa kwa Rais Samia kuwa miradi hiyo itakamilishwa kwa kasi kubwa kama ilivyokusudiwa.

Aliwaomba watumishi serikalini kutoa ushirikiano wa karibu wa kusimamia miradi hiyo kwa uaminifu ili malengo ya Watanzania ya kuinuka kiuchumi zaidi yaweze kuwafikia watu wote.

Alisema kwa upande wa wananchi wa Kijiji cha Buigiri, Wilaya ya Chamwino, wataendelea kumkumbuka na kumuenzi Hayati Dk. Magufuli kwa maamuzi yake magumu ya kusitisha sherehe za Uhuru na fedha zake kutumika kujenga Hospitali ya Uhuru kijijini hapo.

Alisema uamuzi huo ni kitendo cha kuthubutu ambacho leo Watanzania wanajivunia hospitali hiyo ambayo kwa Mkoa wa Dodoma imepata heshima kutokana na uwapo wa makao makuu ya serikali ambayo wananchi wanapata huduma ya matibabu.

Pia alisema Hayati Rais Magufuli atakumbukwa kwa moyo wake wa kuwajali watu wa hali ya chini na wafanyabiashara ndogo ambao walikuwa wakibughudhiwa na mgambo kila wakati na kuwasababishia wengine kupoteza bidhaa na hata mitaji yao.



Mkurugenzi wa Elimu Maalumu Wizara ya Elimu, Magrert Mathoya, akizungumza na wadau wa elimu jumuishi (hawapo pichani) kwenye mkutano wa kuhitimisha mradi wa kuwahudumia watoto wenye ulemavu uliokuwa ukisimamiwa na shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Sheshire uliofanyika juzi Dodoma, kushoto ni Meneja wa Kanda ya Afrika Mashariki kutoka Shirika la Leonard Sheshire, Catherine Alejo, (kulia) Ofisa Elimu Maalum, Aghes Mwingira na Mratibu wa elimu jumuishi Wizara ya Elimu, Asha Mbwambo. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Wakulima zabibu wapewa angalizo mavuno

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAKULIMA wa zao la zabibu mkoani Dodoma, wametakiwa kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa zao hilo, ili kuepuka kupotea kwa wingi likiwa shambani kipindi cha msimu wa mavuno.

Hayo yalisemwa na mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), kituo cha Makutupora, Andekelile Mwamahonje, wakati akielezea umuhimu wa kuzingatia taratibu za kulima zao hilo.

Andekelile alisema vitu vinavyohitajika kuvuna mazao mengi ni pamoja na kuzingatia elimu ya uandaaji shamba, kupanda na hadi inapofika msimu wa kuvunwa.

Mwamahonje alisema kuna baadhi ya wakulima hawajui matumizi ya mbegu bora, wakishindwa kutambua hilo mwisho wa siku wanapata shida kadri zabibu inavyoendelea kukua.

Alisema wanapaswa kuzingatia elimu wanayopewa na wataalamu ili kufanya kilimo cha zabibu chenye tija.

"Kuna baadhi ya hatua wakulima hawazijui ndio maana huwa tunaenda kutoa elimu kwa wakulima katika baadhi ya maeneo ili kuwasaidia wasipoteze zabibu nyingi shambani kipindi cha mavuno," alisema Mwamahonje.

Alisema tayari walishatembelea Halmashauri ya Chamwino, Bahi, kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima ili wafanye vizuri msimu wa kilimo.

Alisema moja ya mikakati ya kituo hicho ni kutoa elimu kwa wakulima wa zao la zabibu ambalo ni la biashara ili kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo chenye tija.

Alisema zabibu ni zao la biashara na linapendwa na watu wengi na kwamba ni vyema kila mkulima akiwa na elimu ya namna ya kutunza zao hilo tangu mwanzo wa upandaji hadi msimu wa kuvunwa.

Mwamahonje, alisema wakulima wanapaswa kuzingatia maelekezo ya utunzaji kutokea msimu wa kupanda hadi mavuno kwa sababu wakifanya hivyo itawasaidia kwa kiasi kikubwa kupata mavuno mengi kipindi cha kuvunwa.

"Tunaomba wakulima wazingatie elimu inayotolewa na kituo cha utafiti wa kilimo, tunahitaji kuona wakulima wa zao hilo mkoani hapa wanapiga hatua katika kilimo hicho," alisema Mwamahonje.

Alifafanua kuwa zao la zabibu halifanani na mazao mengine na inachukua muda mrefu, mkulima anapaswa kufuata taratibu ambazo watafiti wameelekeza ambazo zitawapa manufaa makubwa katika kilimo.

Naye Mary Stephene, kutoka Idara ya mbegu alisema kituo hicho kimekuwa kikifanya jitihada za kuhakikisha wakulima wa zao hilo mkoani hapo wanakuwa mfano wa kuigwa na wakulima wengine.

Alisema Dodoma ni mkoa pekee ambao zao hilo linalimwa misimu miwili, wakulima wanatakiwa kupata elimu mara kwa mara ya uandaaji mpaka uvunaji.



# DC Chunya ataka watoto kupewa elimu ya zebaki

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

MKUU wa Wilaya Chunya mkoani Mbeya, Mayeka Simon, ameitaka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Nyanda za Juu Kusini kufikisha elimu ya matumizi kemikali hususani zebaki kwenye shule za msingi na sekondari ili watoto wanaojihusisha na machimbo kuacha mara moja.

Mayeka aliyasema hayo juzi, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku mbili yanayoendeshwa na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Nyanda za Juu Kusini Mkoa wa Mbeya, ambayo yalifanyika wilayani hapo kwa ajili ya kutoa elimu ya matumizi ya kemikali hususani ya zebaki ambayo yanaathiri afya za wananchi.

Alisema kundi la watoto nalo linajihusisha na shughuli za uchimbaji madini na bila kujua athari zake hawachukui hatua zozote na kwamba mafunzo hayo yatakuwa msaada. "Wachimbaji wengi wilayani Chunya hawana vifaa vya kisasa kwa ajili ya uchimbaji wengi wao wanatumia zebaki kupata dhahabu jambo ambalo linaathiri afya zao watoto nao ni kundi ambalo halichukui tahadhari yeyote," alisema Mayeka.

Alisema elimu ya matumizi ya kemikali kwenye shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu itasaidia kuokoa afya za wananchi ikiwamo, wachenjuaji, wenyeviti wa mitaa ambao wanasimamia sheria na pamoja na wasafirishaji wa kemikali.

Mayeka alipiga marufuku kwa wazazi pamoja na walezi kuacha tabia ya kuwatumikisha watoto kwenye shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu kwa kuwa kemikali za zebaki ambazo zinatumika kuchenjua zina madhara ya moja kwa moja kiafya.

Alisema kuwa elimu ya matumizi sahihi ya kemikali kwa wachimbaji wa madini ya dhahabu na wachenjuaji wa madini ni muhimu kutokana na kusaidia kemikali kutosambaa maeneo ya makazi na kuhatarisha afya za wananchi na viumbe hai wengine na pia ingewafikia watoto shuleni ingesaidia kuwaepusha na madhara yanayoweza kuwapata hapo baadaye.

Akiwasilisha mada ya madhara ya kemikali kwa washiriki wa mafunzo Mkemia, Sitoni Nasira kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Nyanda za Juu Kusini aliwataka wachimbaji wa madini ya dhahabu wilayani hapa kuacha kufanyakazi kwa mazoea badala yake kujikinga na madhara ya kemikali na kueleza kuwa madhara hayo huathiri figo, ubongo na mfumo mzima wa upumuaji.

Alisema madhara ya kemikali zinazotumika kuchenjulia madini ya dhahabu ikiwamo zebaki zikitumika vibaya zinaweza kuleta madhara kwa mtumiaji ambayo huunguza ngozi, kuharibu mfumo wa uzazi, kuharibu mfumo wa homoni, kansa na kuhatarisha vinasaba (DNA).

Aliwashauri wachimbaji kufuata taratibu zote zilizowekwa na ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuepusha madhara na kuwashauri wanapokumbana na vikwazo mbalimbali kufika Ofisi ya Kanda kupata ushauri.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo, Jerry Brayson, alisema mafunzo hayo yamekuja wakati muafaka na yatawasaidia kufanyakazi kwa tahadhari kubwa tofauti na walivyozoea kufanya kazi kwa mazoea.

## Kutojua sheria chanzo migogoro wakulima, wafugaji

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KUTOFAHAMU sheria ya ardhi kumetajwa kuwa ni miongoni mwa sababu inayosababisha migogoro ya wakulima na wafugaji kwenye jamii kutokana na watu kutojua mipaka yao ya kudai haki au kuitekeleza sheria hiyo.

Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, waliyasema hayo, wakati wakizungumza na waandishi wa habari wakati wa warsha kutambulisha mradi wa utetezi wa upatikanaji wa matumizi bora ya ardhi iliyoendeshwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la MIICO kwa ufadhili wa mashirika ya nje ya DKA na Welthaus kutoka Austria.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sangambi, Lusekelo Lwesya, alisema bado kuna tatizo katika suala la usuluhi wa migogoro ya ardhi hasa katika jamii za wakulima na wafugaji na wasimamizi wa sheria wanapaswa kuyasaidia makundi hayo.

Alisema kupitia mradi huo anaamini elimu inayoendelea kutolewa itasaidia kupunguza migogoro kwenye vijiji vya Kata ya Sangambi, baina ya wakulima, wafugaji pamoja na wachimbaji wa madini ya dhahabu.

"Kuna tatizo la uporwaji wa ardhi baina ya wakulima na wafugaji kutokana na baadhi yao kujimilikisha kimabavu ardhi kwa sababu ya uwezo wa kifedha hivyo baadhi ya mamlaka kutokuwa na sauti katika kulisimamia jambo hilo," alisema Lwesya.

Baadhi ya wakazi wa Sangambi, Nikutusya Kahonga alisema elimu ya sheria ya ardhi inahitajika ili kukabiliana na migogoro na namna bora ya kudai haki kupitia vyombo vya sheria.

Alisema kwa sasa kundi kubwa linaloathirika na masuala ya ardhi ni wakulima, baadhi ya wawekezaji, wachimbaji na wafugaji wenye uwezo kifedha hupora ardhi na kwamba wanapofika kwenye mamlaka hakuna hatua zozote zinazochukuliwa.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mayeka Simon, aliwatakata wananchi wilayani humo, kuhakikisha wanashirikiana vyema na Shirika la MIICO, kudhibiti na kutoa elimu ya matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro kati ya wakulimu na wafugaji.

Mayeka alisema serikali itahakikisha inashirikiana na shirika hilo bega kwa bega kuhakikisha wananchi wanapata elimu hiyo ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Kwa upande wake, Ofisa Mradi wa Shirika la MIICO, Gloria Mdindile, alisema lengo la mradi huo ni kuwezesha wananchi kuwa na uhakika wa chakula na kujijengea uelewa jamii juu ya masuala ya usimamizi wa ardhi na utawala wa rasilimali ardhi pamoja kuwapa uelewa wa Sheria ya Ardhi Namba 5 ya mwaka 1999 ya Sheria ya Vijiji.

Mdindile alisema mradi huu wa utetezi wa upatikanaji wa ardhi bora kwa wazalishaji wadogo ili kuwa na uhakika wa chakula kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Akiwasilisha taarifa ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa Wilaya ya Chunya, Ofisa Mipango Miji, Sunday Mwakalebela, alisema kupitia na mradi huu unaoendeshwa na shirika hilo utasaidia kutatua baadhi ya migogoro miongoni mwa jamii.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Bujesi, Kata ya Kasumulu, wilayani Kyela katika mkoa wa Mbeya, wakiangalia shughuli za ujenzi wa Shule ya Msingi Kasumulu baada ya kujitoa kufikia hatua hiyo, huku Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Kinanasi (hayupo pichani) akitoa mchango wa Sh. 500,000 kusaidia ukamilishaji ujenzi wa vyumba sita vya madarasa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mil. 375/- za mapato ya ndani wapewa mkopo wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imetoa Sh. milioni 375 kwa ajili ya mikopo ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Akizungumza na Nipashe kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, Ofisa Maendeleo, James Sunge, alisema wameendelea kutekeleza sheria inayotaka asilimia 10 ya mapato ya ndani itolewe kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Sunge alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha fedha zaidi ya milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya kuviwezesha vikundi hivyo ambavyo vimewasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo na kuepukana na utegemezi.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo, akiwamo Rusia Braison, ambaye ni mjane alisema umemwezesha kuendesha biashara yake ya mama ntilie pamoja na uuzaji matunda na mboga hali iliyochangia kumudu gharama za kuhudumia familia.

"Biashara hii imesaidia kuajiri na wengine ambao nao wamejikwamua kiuchumi ukilinganisha na ilivyokuwa awali, lakini mimi pia anasomesha watoto kwenye shule za mchepuo kwa Kiingereza," alisema Rusia.

Mnufaika mwingine, Jackline Fanuel, ambaye ni fundi nguo, alisema mkopo wa halmashauri umemsaidia kupata mtaji wa kupanua biashara yake kwa kukidhi mahitaji ya wateja ambao wanahitaji bidhaa mbalimbali.

Mwisho

**"Biashara hii imesaidia kuajiri na wengine ambao nao wamejikwamua kiuchumi ukilinganisha na ilivyokuwa awali, lakini mimi pia anasomesha watoto kwenye shule za mchepuo kwa Kiingereza," alisema Rusia.**





# Mwera walalamika kukosa maji miezi 3

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wa Shehia ya Mwera Mtofaani Unguja, wamesema kupasuka kwa bomba la maji kumesababisha kukosa huduma ya majisafi na salama kwa miezi mitatu sasa.

Walisema hali hiyo imesababisha kupata usumbufu mkubwa kusaka huduma hiyo muhimu kwa maisha ya kila siku.

Wakizungumza jana na viongozi wao wa Jimbo la Welezo, wananchi hao walisema kutokana na uwezo wao wa kifedha kuwa mdogo, wameshindwa kulifanyia matengenezo bomba hilo.

Asha Makame, aliwaomba viongozi wa jimbo hilo kuwasaidia kulifanyia matengenezo ili wapate huduma ya maji hasa kipindi hiki cha kuelekea mwezi wa Ramadhani.

Alisema wanategemea maji ya kugawiwa ambayo hutolewa na baadhi ya wananchi wenye visima, lakini hayatoshelezi.

Aidha, alisema gharama za matengenezo yote ya mabomba yaliyopasuka pamoja na mafundi na vifaa ni shilingi 700,000, hivyo waliwataka viongozi wa jimbo kuwasaidia kumudu gharama hizo.

Naye Mbunge wa Jimbo la Welezo, Maulid Saleh Ali, aliwataka wakazi wa jimbo hilo kutoa taarifa mapema za changamoto zinazowakabili kwa viongozi wao ili kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mbunge huyo aliahidi kuitatua changamoto hiyo kwa muda mfupi ili wananchi kupata huduma ya majisafi na salama bila ya usumbufu.

**Wakizungumza jana na viongozi wao wa Jimbo la Welezo, wananchi hao walisema kutokana na uwezo wao wa kifedha kuwa mdogo, wameshindwa kulifanyia matengenezo bomba hilo. Asha Makame, aliwaomba viongozi wa jimbo hilo kuwasaidia kulifanyia matengenezo ili wapate huduma ya maji hasa kipindi hiki cha kuelekea mwezi wa Ramadhani.**

# ACT-Wazalendo yashinda Pandani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeshinda katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani kwa nafasi ya uwakilishi, mgombea wake Omar Faki Hamad, alipata kura 2,361 na kumshinda mpinzani wake kutoka CCM, Muhammed Juma Ali, aliyepata kura 1,934.

Uchaguzi huo uliofanyika juzi, umetokana na aliyekuwa Mwakilishi mteule wa jimbo hilo, Abubakar Khamis wa ACT-Wazalendo kufariki dunia mwaka jana. Ushindi huo unaiwezesha ACT kuwa na majimbo manne.

Katika uchaguzi huo kura zote halali zilizopigwa ni 4,500 na 56 zilikataliwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kumtangaza Omar Faki kuwa mshindi.

Akitangaza matokeo hayo Msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo la Pandani, Khamis Abdalla Hassan, alieleza kuwa uchaguzi huo ulikuwa wa huru na haki.

"Kwa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha Sheria ya Uchaguzi ya Namba 4 ya mwaka 2008, namtangaza rasmi Omar Fakih Hamad kuwa Mwakilishi mteule wa Jimbo la Pandani," alisema Abdalla.

Wagombea wengine waliogombea nafasi hiyo ni Massoud Ali Said CUF aliyepata kura 79, Ali Jabir Khamis ADC (33), Ali Hamad Omar ADA-TADEA (25), Said Hamad Ali Demokrasia Makini (28), Khamis Faki Mgau NRA (19), Mohammed Sharif Khamis URND (13), Asha Foum Ali UDP (2) na Abdalla Ali Ahmed AFP (6).

Akizungumza na waandishi wa habari Faki alisema atahakikisha anatekeleza ahadi alizowaahidi wananchi wa jimbo hilo katika kuwaletea maendeleo.

Katika hatua nyingine, ZEC imemtangaza Salama Rajab Masinga kuwa Diwani wa wadi ya Kinuni kutoka CCM, baada ya kushinda katika uchaguzi mdogo wa wadi hiyo na kupata kura 2,374.



Ofisa Mdhamini Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, Ahmed Abubakar Mohamed, akizungumza na wadau wa haki za wanawake na watu wenye ulemavu, kwenye hafla ya uzinduzi wa mwongozo kwa ajili ya makundi hayo, kuelekea uchaguzi mkuu ujao, hafla hiyo ilifanyika kiwanda cha Mafuta ya Makonyo Wawi Chakechake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi Pemba watakiwa kujikita masomo ya sayansi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANAFUNZI wa shule za sekondari Kisiwani Pemba, wameshauriwa kujikita katika masomo ya sayansi yanayoendana na fani ya ardhi ili kujiweka tayari kuingia katika soko la ajira na kuziba pengo la mahitaji ya wataalamu hao.

Ushari huo ulitolewa na Ofisa Utafiti Ofisi ya Mtathmini Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Zubeir Said Rashid, kwa nyakati tofauti huko Kisiwani Pemba, wakati akizungumza na wanafunzi wa shule za sekondari za Madungu, Uweleni na Mohammed Juma Pinduwa Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema Zanzibar imekabiliwa na uhaba wa wataalamu wa fani ya ardhi kwa kiwango kikubwa na kufanya ajira hizo kuchukuliwa na wataalamu kutoka sehemu moja ya Muungano wakati rasilimali ya upatikana wataalamu hao ipo Zanzibar.

Alieleza kutokana na upungufu huo, kuna haja kubwa kwa wanafunzi kusoma masomo hayo kutokana na umuhimu wao juu ya mahitaji ya sekta hiyo ambayo inakua.

"Wanafunzi eleweni hii fani ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa kwani kabla ya kupitisha miundombinu ya aina mbalimbali, kunahitajika tathmini ya rasilimali mbalimbali zilizopo kwanza kabla ya kufanyika ujenzi husika," alieleza.

Zubeir alisema kuwapo kwa watathmini wazuri wa rasilimali kunaiwezesha serikali kuondoa matumizi ya fedha kiholela na hatimaye kupunguza gharama kubwa ya fedha ambazo zinaweza kutumika kwa shughuli zingine.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inahitaji wataalamu zaidi kutokana na uhaba wao na kwamba waliopo Zanzibar sio zaidi 40, na kati yao wakiwa karibu na kumaliza muda wa utumishi wao na wenye shahada ya kwanza ya fani hiyo sio zaidi ya 10.

"Kutokana na upungufu huu wa watathmini kwa Zanzibar, wataalamu wengi wanaofanya kazi hizo hapa Zanzibar wanatoka Tanzania Bara kwani Zanzibar zipo kampuni tatu tu zilizosajiliwa wakati kwa wenzetu bara wanazo kampuni ni zaidi ya 43, hivyo fedha nyingi kwenda huko," alisema.

Naye Ofisa kutoka Kamisheni ya Ardhi Pemba, Said Saleh Makame, alieleza utathmini wa ardhi ni muhimu kwa Taifa lolote na hali hiyo inasababisha kutumia ardhi endelevu kwa vile unakuwapo mpangilio na hiyo pia itaenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu.

Mratibu wa Taasisi ya Elimu Zanzibar Ofisi ya Pemba, Asha Soud Nassor, aliwataka wanafunzi kutochagua masomo, na kuwa kila somo lina faida yake na kuna upungufu wa watendakazi kwa baadhi ya maeneo muhimu ndani ya serikali.

Wanafunzi hao walisema wameupokea ushauri huo na umewazindua kwa kiasi kikubwa na wataelekeza akili zao kwenye masomo hayo.

Mwanafunzi Mzee Moh'd Faki wa kidato cha sita Shule ya Sekondari Madungu, aliiomba serikali kufikiria utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa fani hizo ili iwe chachu kwa wanafunzi kujiunga na vyuo vinavyotoa masomo hayo.

HABARI KIMATAIFA

# Obama alimlilia bibi yake aliyefariki Kenya

**Nairobi,** KENYA

RISALA za rambirambi zimekuwa zikitolewa kufuatia kifo cha Mama Sarah Obama (99), ambaye ni bibi yake rais wa zamani wa Marekani, Barrack Obama.

Sarah, alifariki dunia jana asubuhi katika hospitali mojawapo iliyopo Magharibi mwa Kenya.

Rais Obama alipopewa taarifa ya kifo cha bibi yake, alituma salamu za rambirambi akisema: Atazikwa Jumanne kabla ya adhuhuri na mazishi yatafuata kanuni za kiislamu."

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alimwomboleza kama Sarah, akimtaja mwanamke mwadilifu na kigezo cha maadili ya kifamilia.

Waziri Mkuu wa zamani wa Kenya, Raila Odinga alimpongeza Sarah Obama kwa kuwa nguzo ya familia baada ya kifo cha mume wake.

"Alitumia nafasi ya mjukuu wake kuimarisha masomo ya watoto wa kike na kukabiliana na maovu katika jamii kupitia wakfu wake," alisema Odinga.

Mtoto wa marehemu, Marsat Onyango alisema mama yake alifariki dunia majira ya alfajiri jana, akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Chuo cha Jaramogi Oginga Odinga iliyopo Kisumu.

"Alifariki asubuhi. Tunasikitika," alisema Onyango akizungumza na Shirika la Habari la Associated Press (AP).

Dada yake Rais Obama, Auma Obama, aliandika katika ukurasa wake wa Twitter jana na kusema: nimevunjika moyo, nilibarikiwa kuwa naye kwa muda mrefu."

Gavana wa Kisumu, Anyang Nyong'o alipotuma salamu za rambirambi alisema Sarah, atakumbukwa na watu wa kijiji cha Kogelo hususan kwa jitihada zake za kuinua elimu kwa wasichana na yatima.

Sarah Obama, alifariki baada ya kuugua kwa muda mfupi kutokana na ugonjwa ambao haukutajwa.

BBC/AP




Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama, akifurahia jambo akiwa amemkumbatia bibi yake, Sarah Obama (kulia), alipowasili kijiji cha Kogelo, Magharibi mwa Kenya, Julai 16, mwaka 2018. Bibi Sarah amefariki dunia jana akiwa na umri wa miaka 99, akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Jaramogi Oginga Odinga. **PICHA: MAKTABA**

# Maelfu wayakimbia makazi Msumbiji

**Palma,** MSUMBIJI

MAELFU ya watu wamekuwa wakijaribu kwa njia zote kuyatoroka makazi yao, Kaskazini Mashariki mwa Msumbiji, inayokabiliwa na mashambulizi makubwa ya wanajihadi tangu Jumatano wiki iliyopita na kuua raia wengi.

Mwishoni mwa wiki, serikali ya Msumbiji ilithibitisha kwamba watu wasiopungua saba, waliuawa katika shambulio la Ijumaa, wakijaribu kutoroka kutoka hoteli walikokuwa wamekimbilia.

Shambulio la kwanza lilikuwa dhidi ya mji mdogo wa Palma, ulio kilometa kumi tu kutoka eneo la gesi linalosimamiwa na kampuni ya Ufaransa ya TOTAL, ambayo imeanzisha mradi mkubwa wa dola bilioni 20, utakaoanza kutumika mwaka 2024.

Mji wa Palma ulianguka mikononi mwa makundi haya yenye silaha siku ya Ijumaa jioni, baada ya zaidi ya saa 48 ya mapigano.

"Zaidi ya watu 100 wametoweka," mtafiti Martin Ewi, kutoka Taasisi ya Mafunzo ya Usalama huko Pretoria, aliliambia Shirika la Habari la AFP, akibaini kwamba hali bado ni tete katika mji huo.

Wanajihadi, ambao wametangaza kuungana na kundi la Islamic State (IS) na ambao kwa zaidi ya miaka mitatu, wameendelea kutishia maisha ya wakazi wa jimbo lenye waislamu wengi la Cabo Delgado, linalopakana na Tanzania.

Inadaiwa walifanya mashambulizi ya kushtukiza kwa wakati mmoja Jumatano wiki iliyopita, alasiri kutoka eneo la pande tatu na kusababisha hofu kwa wakazi wapatao 75,000.

Mashahidi waliliambia shirika lisilo la kiserikali la Human Rights Watch kwamba, walifyatua risasi "kila mahali, wakilenga watu na majengo", na kuacha miili ya watu barabarani.

"Vitendo vyao vilisababisha mauaji ya makumi ya watu wasio na ulinzi," Kanali Omar Saranga, msemaji wa Wizara ya Ulinzi, alisema katika mkutano na waandishi wa habari.

Wengine wamekimbilia kuelekea misitu ya karibu, wengine kuelekea fukwe wakitumia usafiri wa boti. Huku baadhi wakiondoka kwa miguu au kwa magari kwenda kwenye eneo la gesi.

RFI

# Uganda kutengeneza chanjo ya corona

**Kampala,** UGANDA

SERIKALI ya Uganda, imeanza mchakato wa kutengeneza chanjo kwa ajili ya ugonjwa wa Covid-19 kama mataifa mengine duniani.

Mwaka jana, Rais Yoweri Museveni alisema wanasayansi wanajaribu kufanya utafiti kuanza kutengeneza chanjo yao na tiba ya Covid-19 ambayo tayari iko kwenye majaribio.

"Ninafanya kazi na watu wangu kuanza kutoa chanjo yetu, sio kwamba tumekaa tu kusubiri watusaidie, tumechelewa lakini sasa tumeanza na chanjo yetu itakwenda kote duniani," alisema Rais Museveni.

"Tutaanza kufanyia majaribio panya mwezi Juni, mwaka huu, kuona kama ina madhara na baadaye Augosti tutafanyia majaribio nyani na kusubiri kuthibitishwa na WHO."

Rais Museveni alitoa kauli hiyo wakati alipodungwa sindano ya chanjo ya Covid-19 ya Astra Zeneca pamoja na mkewe Janet Museveni, katika ikulu ya Rais Nakasero, mjini Kampala.

Museveni alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kupata chanjo na kwamba haina madhara.

BBC

# Kesi ya George Floyd yaendelea kusikilizwa

**Minneapolis,** MAREKANI

USIKILIZWAJI wa kesi kutoka pande zote za utetezi na mashtaka wa shauri la polisi wa zamani wa jiji la Minneapolis, Derek Chauvin, ambaye anashtakiwa kwa mauaji ya Mmarekani mweusi George Floyd, umeendelea.

Tukio hilo la mwaka jana, lilizusha maandamano kote duniani.

Kesi hiyo ambayo itasikilizwa na watu 12 wanaounda Baraza la Mahakama wanatarajia kusikiliza ushuhuda katika kesi hiyo inayotarajiwa kuchukuwa mwezi mmoja kukamilika.

Ofisa huyo wa polisi ambaye ni mzungu alipinga mashtaka yote yanayomkabili yanayohusu mauaji ya mwanaume huyo mwenye asili ya kiafrika, George Floyd.

Alijitetea kwa kusema alichokifanya kiliendana na mafunzo ya kipolisi aliyopewa wakati alipokuwa akimkamata Floyd.

VOA

# SOUTHGATE AONA UBORA KIKOSI CHA ENGLAND

**TIRANA, Albania**

GARETH Southgate ameona kuimarika kwa kiwango cha kikosi cha England baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Albania kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar.

'Simba Watatu' hao walitoka kupata ushindi wa 5-0 dhidi ya San Marino na kuwa kileleni mwa msimamo wa Kundi I, baada ya ushindi huo wa Jumapili dhidi ya Albania.

Nahodha Harry Kane alimaliza ukame wa mechi sita bila kufunga bao kwa nchi yake wakati alipofunga kwa kichwa kabla ya Mason Mount kufunga la pili.

Baadaye Kane na Phil Foden mashuti yao yaligonga mwamba wa lango la Albania na walionekana kama wangeweza kuondoka na ushindi mnono kwenye mchezo huo.

Na sasa kocha huyo wa England, Southgate alionyesha kukunwa na kiwango cha kikosi chake hicho.

"Ilikuwa ni vigumu kuzoea uwanja na kusukumiza mashambulizi mbele, lakini tuliweza kupata ushindi," alisema Southgate akiiambia ITV Sport.

"Baada ya dakika 25 tulibadilisha mchezo hasa kwenye safu ya kiungo na tulionekana kuwa hatari zaidi.

"Tulikuwa na wakati mzuri zaidi kipindi cha pili. Kwani tulikuwa na nafasi nyingi zaidi za kufuzu na tungeweza kupata bao la tatu na kumaliza kabisa mchezo.

"Sasa naona mabadiliko kwenye kikosi, kinaimarika na kucheza vizuri zaidi, nina imani tutaendelea kuwa kwenye kiwango hicho."



# DEMBELE AMKUNA KOCHA UFARANSA

**NUR-SALTAN, Kazakhstan**

OUSMANE Dembele anaimarika kwa kuwa kwenye "njia sahihi", kocha Didier Deschamps amesema baada ya winga huyo wa Barcelona kufunga bao wakati Ufaransa ikishinda 2-0 dhidi ya Kazakhstan.

Baada ya sare dhidi ya Ukraine kwenye mchezo wa kwanza wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, mabingwa hao watetezi walipaa kileleni mwa msimamo wa Kundi D kutokana na ushindi huo wa Jumapili.

Dembele alifunga bao la uongozi, kabla ya mlinzi wa Kazakhstan, Sergiy Maliy kujifunga, huku Kylian Mbappe alikosa penalti dakika ya 75.

Huo ulikuwa ni ushindi wa saba mfululizo kwa Ufaransa kucheza ugenini ikiwa ni rekodi bora zaidi tangu Januari 1990 hadi Oktoba 1991.

Dembele, ambaye 'amekifufua' kwa kiwango chake kule Barca msimu huu baada ya kusumbuliwa na majeraha ya muda mrefu kwenye dimba la Camp Nou, alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia na alitolewa nje dakika ya 90 nafasi yake ikichukuliwa na Kingsley Coman.

Alipoulizwa kuhusu kiwango cha Dembele, Deschamps aliwaambia waandishi wa habari: "Alifanya vitu vya kuvutia.

"Ousmane amethibitisha kwamba yupo kwenye njia sahihi sasa. Ana uwezo wa kubadilisha matokeo kwa jitihada zake.

"Kwa hakika sasa yupo kwenye kiwango cha kuvutia na anaonekana kuimarika vizuri."

# MANCINI: HAIKUWA RAHISI KUIFUNGA BULGARIA

**SOFIA, Bulgaria**

ITALIA hawakuwa kwenye kiwango chao bora dhidi ya Bulgaria Jumapili, lakini kocha Roberto Mancini hakutarajia kitu chochote tofauti kutoka kwenye kikosi chake hicho.

Mancini akiwa na Italia sasa amefikisha mechi 24 bila kupoteza akizidiwa moja tu na Marcello Lippi na sita kwa rekodi ya kuongoza mechi nyingi bila kupoteza inayoshikiliwa na kocha Vittorio Pozzo aliyoiweka mwaka 1930.

Italia ilipata ushindi huo kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar kwa mabao ya Andrea Belotti na Manuel Locatelli.

Ushindi huo umeifanya Italia ambayo iliifunga Ireland Kaskazini kwenye mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo ya kufuzu, kuwa pointi sawa na Uswisi kileleni mwa Kundi C.

Italia kwenye mchezo huo ilitawala kwa asilimia 67.6 na ilipiga mashuti 22, huku 12 yakizuiwa na sita yalilenga lango.

Wakati safu ya ushambuliaji haikuwa na makali sana, lakini kwa upande wa ulinzi walikuwa imara na kufikisha mchezo wao wa sita mfululizo bila nyavu zao kutikiswa.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Mancini aliiambia RAI Sport: "Mechi zote ni ngumu hasa unapocheza na timu kama Bulgaria ambayo ina staili ya 'kupaki basi' na kusubiri kwa mashambulizi ya kushtukiza.



"Sio rahisi kuwapenya na kutengeneza mashambulizi, ni jambo kubwa na ilikuwa hivyo kwenye mchezo huu."

## DEFOE AMWAMBIA KANE AONDOKE SPURS

**LONDON, England**

HARRY Kane lazima aondoke Tottenham Hotspur kama anataka kushinda mataji, kwa mujibu wa Jermain Defoe.

Kane mkataba wake na Spurs unamalizika Juni 2024, lakini nahodha huyo wa England ameshabainisha kwamba, ataamua majaliwa yake baada ya michuano ya Euro 2020.

Defoe anaamini kwamba, Straika huyo mwenye umri wa miaka 27 anatakiwa kuipa kisogo timu yake hiyo ya utotoni kama ana njaa ya kutwaa mataji.

Mchezaji huyo wa Rangers na nyota wa zamani wa Tottenham, ameiambia talkSPORT: "Kama ungeniuliza mimi swali hili miaka michache iliyopita, ningesema anatakiwa kubaki pale, kwa kile alichokifanya kwenye klabu yake, yeye ni gwiji.

"Tangu nimekuja hapa Rangers, nimeona kwamba, anatakiwa kucheza kwenye klabu kubwa, na umuhimu wa kucheza kwenye klabu kubwa ni kwamba atashinda katika kila mechi.

"Unatakiwa kushinda na kutwaa mataji, vinginevyo si jambo nzuri kwake. Wakati unaposhinda mataji ni jambo zuri zaidi kwa mchezaji binafsi.

"Kama Harry Kane anataka hilo na anataka kushinda mataji, lazima aondoke pale Spurs na sasa inaonekana wazi kwamba anatakiwa kuondoka."

## MODRIC AJIWEKEA REKODI CROATIA

**ZAGREB, Croatia**

LUKA Modric amevunja rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi katika kikosi cha timu ya Taifa ya Croatia.

Mchezaji huyo bora wa Kombe la Dunia mwaka 2018, amevunja rekodi hiyo kwa kufikisha mechi 135 alizocheza kwa kikosi hicho.

Modric amevunja rekodi hiyo katika mchezo dhidi ya Cyprus siku ya Jumamosi ambapo ilikuwa inashikiliwa na mlinzi wa zamani wa Shakhtar Donetsk, Darijo Srna.

Modric aliitwa kwa mara ya kwanza katika kikosi cha Croatia mwaka 2006, na tangu hapo amefanikiwa kucheza mechi 135 akifunga mabao 16 katika mashindano yote.

Mchezaji huyo aliisaidia Croatia kutinga fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2018 ambapo walifungwa na Ufaransa kwa mabao 4-2.





# ARSENAL

## YAMFIKIRIA FEKIR BADALA YA ODEGAARD

**LONDON, England**

ARSENAL imeweka wazi nia yake ya kutaka kumsajili, Nabi Fekir kuwa kama mbadala wa Martin Odegaard wakati wa majira ya joto, kwa mujibu wa Sky Sport.

'Washikabunduki' hao wamekuwa wakivutiwa na mchezaji huyo raia wa Ufaransa kwa muda mrefu na walimtaka kabla hajatua Real Betis akitokea Lyon mwaka 2019.

Fekir alitumia miaka miwili iliyopita huko Hispania na sasa Arsenal wapo kwenye rada za kumsajili kiungo mshambuliaji huyo wakati wa majira ya joto.

Mwanzoni Arsenal waliweka dhamira ya kufanya jitihada za kumbakisha Odegaard, ambaye anatarajia kurejea Real Madrid baada ya muda wake wa kucheza kwa mkopo kumalizika pale Emirates mwishoni mwa msimu huu.

Klabu hiyo ya Kaskazini mwa London haina kipengele kwenye mkataba wao na Odegaard ambacho kinawaruhusu kumnunua moja kwa moja, lakini walikubaliana na Madrid watafanya mazungumzo mwishoni mwa msimu.

Arsenal walikuwa wanapendelea kumsajili raia huyo wa Norway kwa mkataba wa muda mrefu, lakini kwa sasa haijawekwa wazi kama Real Madrid watamwachia.

Baada ya kushindwa kutua Liverpool mwaka 2018, Fekir mwishowe aliachana na Lyon na kwenda Real Betis msimu uliofuata.

Alimaliza msimu wake wa kwanza akiwa na mabao saba huko Hispania, huku akifanikiwa kutoa pasi za mwisho nne katika mechi 31, lakini pia amefanikiwa kufunga mabao matatu tu msimu huu kwenye mashindano yote na kutoa pasi za mwisho tano kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Manuel Pellegrini.

## KWA UFUPI

**KANE ASHAURIWA KUONDOKA**

MCHEZAJI wa zamani wa Tottenham, Jermain Defoe, anaamini kuwa mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, anahitajika kuondoka hapo Spurs kama anataka kushinda mataji. (**Talksport**)

**UNITED BADO YAMTAKA DEMBELE**

KLABU ya Manchester United ilishindwa kumsajili Ousmane Dembele mwenye miaka 22 msimu uliopita, lakini bado imeonyesha nia ya kumsaka mchezaji huyo na ina mawasiliano na watu wake wa karibu. (**Sport**)

**DYBALA KUBADILISHWA NA POGBA**

JUVENTUS ipo tayari kumtumia mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake unakamilika Juni 2022, kama sehemu ya makubaliano ya mabadilishano na kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye miaka 28. (**Football Italia**)

**LLORIS KUBAKI TOTTENHAM**

GOLIKIPA wa Ufaransa, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 34, huenda akasalia Tottenham Hotspur msimu huu, licha ya yeye kutaka kuondoka mwishoni mwa msimu huu. (**Football London**)

**LIVERPOOL YAMTAKA CAKIR**

LIVERPOOL itaandaa kitita cha pauni milioni 15 kujaribu kumsajili golikipa wa Uturuki, Ugurcan Cakir anayechezea klabu ya Trabzonspor, huku RB Leipzig na Sevilla pia zikimnyatia kipa huyo mwenye umri wa miaka 24. (**Express**)

**BELLERIN ATAONDOKA ARSENAL**

MLINZI wa zamani wa Arsenal, Bacary Sagna amesema "hatashangaa" kama beki wa kulia wa Hispania, Hector Bellerin mwenye miaka 26, ataondoka kwa 'Washikabunduki' hao. (**Goal**)

**DEMBELE KUONGEZEWA MKATABA**

BARCELONA inataka kumwongezea mkataba mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri 22, ambapo mkataba wake wa sasa unakamilika mwaka 2022. (**Mundo Deportivo**)

**KALAROV KUSEPA INTER**

NYOTA Aleksandar Kolarov mwenye umri wa miaka 35, huenda akaondoka Inter Milan mwishoni mwa msimu huu, akielekea Bologna ambayo ni moja kati ya klabu tano zinazomwania mlinzi huyo wa zamani wa Manchester City. (**Tuttosport - in Italian**)

**KROOS KUSTAAFU UJERUMANI**

KIUNGO wa kati wa Real Madrid na Ujerumani, Toni Kroos mwenye umri wa miaka 31, yuko tayari kustaafu soka la kimataifa kama watashinda Kombe la Euro 2020. (**Marca**).

**MULLER KUONDOKA BAYERN**

NYOTA wa Ujerumani, Thomas Muller mwenye umri wa miaka 31, ambaye awali alikuwa akiwaniwa na Manchester United, amesema haitakuwa "tatizo kwake" kuondoka Bayern Munich kwa sasa. (**Times**)

**DALOT KUSAJILIWA JUMLA**

MANCHESTER United imeanza mazungumzo na AC Milan kwa ajili ya kumsajili kwa mkataba wa kudumu mlinzi wa klabu hiyo ya Italia mwenye umri wa miaka 22 raia wa Ureno, Diogo Dalot ambaye yuko huko kwa mkopo. (**Metro**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO ASHUKIWA URENO UAMUZI KUSUSIA MCHEZO

●●● Haikubaliki kwa nahodha wa timu ya taifa, hawezi kutupa kitambaa cha unahodha chini na kwenda kwenye vyumba...

**LISBON,** Ureno

KITENDO cha Cristiano Ronaldo kususia mchezo baada ya bao lake kukataliwa hakikubaliki, kwani anatakiwa kuwa mfano bora kwa wachezaji wengine kama nahodha, kwa mujibu wa nyota wa zamani wa Ureno, Fernando Meira.

Ronaldo alifikiri amewapa Ureno alama zote tatu wakati wa mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Serbia Jumamosi, baada ya kupata pasi nzuri kutoka kwa Nuno Mendes na yeye kuubetua kuelekea goli lililokuwa wazi, kipa akitoka.

Lakini wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 akiona mpira umevuka mstari wa goli mlinzi, Aleksandar Mitrovic akautoa na mwamuzi aliruhusu mchezo kuendelea baada ya kushauriana na wasaidizi wake.

Hali hiyo ilimfanya Ronaldo ambaye ni mshindi mara tano wa Ballon d'Or kuonyesha hasira kali na kukitupa kitambaa cha unahodha wake chini na kuondoka uwanjani, huku mechi hiyo ikiendelea na ikamalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Meira anafikiria mchezaji mwenzake huyo wa zamani katika kikosi hicho cha Ureno alikuwa sahihi, lakini anahisi alikwenda mbali sana na kitendo chake kutokana na majukumu yake kama kiongozi wa timu ya taifa.

"Kitendo cha Ronaldo ni cha asili, lakini hakikubaliki kwa nahodha wa timu ya taifa," alisema Meira akiambia Record.

"Hawezi kutupa kitambaa cha unahodha chini na kwenda kwenye vyumba vya kubadilishia nguo wakati mchezo unaendelea. Haikubaliki kwa mchezaji mwenye umuhimu kama yeye.

"Ninaelewa kuchanganyikiwa kwake na ninakubaliana naye kwa sababu bao lake lilikuwa halali, lakini waamuzi wanapaswa kufanya maamuzi, bila VAR, na yeye alipaswa kuonyesha mfano."

HABARI MICHEZO

# MWAKINYO ULINGONI MEI KUWANIA UBINGWA ABU

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA bingwa wa mabara katika uzito wa super welter wa WBF, Hassan Mwakinyo, sasa atapanda ulingoni Mei 28 dhidi ya Brendon Denes wa Zimbabwe kuwania ubingwa wa ABU.

Pambano hilo limepangwa kufanyika kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Dar es Salaam ambapo pia bondia Ibrahim Class atazichapa dhidi ya Evans Takunda Husayihwevhu pia kutoka Zimbabwe katika usiku uliopewa jina la Rhumble in Dar 2.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group Sport, Kelvin Twissa, amesema awali pambano hilo lilipangwa kufanyika Machi 26, mwaka huu na baadaye kuahirishwa kutokana na msiba wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Twissa alisema wanatarajia kuwa na ushindani mkubwa kutokana na mabondia wote kuwa na viwango vizuri katika ndondi za kulipwa.

Alisema bondia Jongo Jongo, atawania ubingwa wa ABU wa uzito wa cruiser dhidi ya bondia wa Nigeria Olanrewaju Durodora.

Kwa mujibu wa Twissa, Jackson Group Sport itaendelea na majukumu yao kuhakikisha kuwa pambano hilo linafanyika kwa kushirikiana na washirika wao Global Boxing Stars na Epic Sports and Entertainment.

"Maandalizi yanaendelea na tunawashukuru washirika wetu wote ambao ni benki ya KCB, Bodi ya Utalii, Onomo Hoteli, DStv, M-Bet, Plus Networks Limited kwa ushirikiano ili kufanikisha pambano hili, ambalo linatarajiwa kuwa na upinzani mkali," alisema Twissa.

Alisema mabondia wamepewa taarifa kuhusiana na mabadiliko ya tarehe mpya ya pambano hilo ambalo lengo kuu ni kumwezesha Mwakinyo kuingia katika orodha ya viwango vya Baraza la Ngumi za Kulipwa Duniani (WBC).

"Mabondia wote wapo katika maandalizi kuelekea pambano hilo ambapo mashabiki watalipa Sh. 50,000 kwa viti vya kawaida na Sh. 200,000 kwa viti maalum. Tikieti hizo zinapatikana kupitia 'app' za nilipe na ontapp," alisema.



Bondia Ibrahim Class (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuelekea pambano lake dhidi ya Evans Takunda Husayihwevhu kutoka Zimbabwe katika usiku uliopewa jina la Rhumble in Dar 2. Pembeni ni Bondia Hassan Mwakinyo ambaye atazichapa na Brendon Denes wa Zimbabwe kuwania ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa Super welter. **MPIGAPICHA WETU**

# Mwajiriwa duka la dawa ashinda milioni 521/- Jackpot SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

UKISIKIA kulala maskini na kuamka tajiri, ndivyo ilivyotokea kwa Abdulaziz Ibrahim, mkazi wa mkoani Tabora na mwajiriwa katika duka la dawa, ambaye amepatia ubashiri wa matokeo ya mechi 13 kwenye Jackpot ya SportPesa na kujishindia shilingi 521,471,360 wiki iliyopita.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya ushindi huo, Ibrahim, alisema kamwe hakufahamu kama angeweza kuibuka mshindi kwa kuwa wakati anabashiri matokeo hayo alikuwa anajaribu tu.

"Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ushindi huu maana wakati nacheza sikutarajia kama nitashinda, ilikuwa kama najaribu bahati kama wengine wengi.

"Niliweza kubashiri kwa usahihi mechi zote 13 na baada ya matokeo nilipokea simu kutoka SportPesa ili kupata taarifa zangu," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas, alisema wanatarajia kumleta mshindi huyo hadharani baada ya kipindi cha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kupita. "Ni matarajio yetu kumleta kwenu baada ya kumtangaza mshindi huyu muda wowote baada ya kumaliza kupindi cha maombolezo ya Hayati John Pombe Magufuli. Ili kumkabidhi pesa zake na kumsikia kiundani ilikuwaje mpaka kuibuka mshindi," alisema Tarimba.

Kuhusu Jackpot mpya baada ya donge hilo nono kunyakuliwa, Meneja Uhusiano wa SportPesa, Sabrina Msuya, alisema kwa sasa tayari imepanda na kufikia dau la shilingi 208,241,480.

"Kwa sasa Jackpot yetu imepanda upya na kufikia kiasi cha shilingi 208,241,480 za Tanzania, ambapo itakuwa wazi kwa wiki hii na kwa atakayebashiri kwa usahihi mechi 13 ataibuka mshindi na kwa watakaobashiri kwa usahihi mechi 10-12 watapata bonasi ya wiki.

"Endapo Jackpot haijapata mshindi kila wiki huongezwa mpaka pale mshindi atakapopatikana," Sabrina aliongeza.

## Ufukweni Tanzania, Burundi ni vita leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, leo itashuka dimbani ikiwa ugenini dhidi ya timu ya Taifa ya Burundi kwenye mchezo wa kuwania kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), mechi itakayochezwa jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Fukwe za Coco.

Katika mchezo huo Burundi watakuwa wenyeji kutokana na kuomba kutumia uwanja huo kwa sababu ya viwanja vya fukwe zao nchini kwao kujaa maji. Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Tanzania, Boniface Pawasa, alisema wako tayari kwa ajili ya mchezo huo wa leo, kuhakikisha wanafanya vizuri ili kufuzu kucheza michuano hiyo inayotarajia kufanyika Mei nchini, Senegal.

Alisema mbali na kufanyia mara kadhaa mazoezi katika Uwanja wa Fukwe za Coco na kuuzoea, wanatambua utakuwa mchezo mgumu na watapambana kupata ushindi katika mechi hiyo.

"Tuko tayari kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Burundi, wachezaji wanatambua majukumu yao na wana kazi ya kusaka ushindi, muhimu ni kupata matokeo mazuri kwa sababu hatuna njia nyingine ya kucheza michuano hiyo ya Afcon," alisema Pawasa.

Naye Kocha wa timu ya Taifa ya Burundi, Bulenge Ally alisema kikosi chake kipo vizuri na fiti tayari kwa ajili ya kuondoka na ushindi katika michezo zote mbili dhidi ya Tanzania ikiwamo mechi ya leo pamoja na Aprili Mosi, ambao utakuwa wa marudiano na wao wakihesabika wako ugenini.

## Ratiba Kombe la FA Zanzibar hadharani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (FA Cup) hatua ya 16-bora, inatarajiwa kuanza kutimua vumbi mapema Aprili 7-10, mwaka huu, imeelezwa.

Bingwa wa michuano hiyo, hupata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Haji Issa 'Kidali', alisema maandalizi yote kuelekea hatua 16-bora ya michuano hiyo yamekamilika na tayari ratiba imeshatolewa kwa klabu ambazo zimetinga hatua hiyo illi kujiandaa mapema.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo iliyotolewa na ZFF kupitia Kamati ya Mashindano, Aprili 7, mwaka huu, itapigwa michezo mitatu katika viwanja mbalimbali vilivyopo mjini Zanzibar na vile vya mikoani, ambapo kwenye Uwanja wa Amaan, Chuoni itavaana na Umoja Mbuzini na katika dimba la Mau A timu ya Black Sailor itapepetana na Mchangani United wakati katika Uwanja wa Kinyasini, New King ikivaana na Taifa Jang'ombe.

# Michezo

Jumanne Machi 30, 2021

Nipashe




RONALDO ASHUKIWA URENO UAMUZI KUSUSIA MCHEZO

HABARI UK 22

WAJE TU...




Wachezaji wa Simba, mshambuliaji Chris Mugalu na beki Kennedy Juma (kulia), wakiwa mazoezini. Jumamosi Simba itaikaribisha AS Vita ya DR Congo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo itakuwa ikihitaji pointi moja tu ili kufuzu robo fainali. **PICHA: MAKTABA YETU**

# CAF YABARIKI POINTI 3 SIMBA ZA AL-MERRIKH

- Yaitupa kapuni rufani yao, uongozi sasa wageukia wito mashabiki kuruhusiwa mechi ya AS Vita...

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka barani Afrika (CAF), limetupilia mbali rufani ya Al-Merrikh ya Sudan, kwa kuwaeleza matokeo ya mechi dhidi ya Simba yatabaki kama yalivyo kutokana na kujiridhisha pasi na shaka kuwa wachezaji wao waliobainika kuwa na maambukizo ya corona vipimo vilikuwa sahihi.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Machi 16, mwaka huu na Al-Merrikh kukubali kipigo cha mabao 3-0, Wasudan hao walikata rufani CAF wakilalamika Simba iliwafanyia hujuma kuwa baadhi ya wachezaji wao wana maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19 ili wasicheze.

Lakini kwa mujibu wa barua ya Jumapili Machi 28, mwaka huu, iliyotumwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Nidhamu ya CAF, Raymond Hack, kwenda kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Soka cha Sudan, imeeleza kuwa Machi 21, mwaka huu, shirikisho hilo lilipokea malalamiko kutoka kwa mwanasheria wa Al-Merrikh, Ahmed Abbass El Hag, wakilalamika kuhusu wachezaji wao kudaiwa wana COVID-19 visivyo halali.

Barua hiyo, imeeleza kuwa malalamiko ya Al-Merrikh kuhusu mechi hiyo namba 101 ya Ligi ya Mabingwa Afrika yalipokelewa na hata hivyo kwa mujibu wa kanuni za sasa na taratibu zinaeleza wazi kuwa "vipimo hivyo vinapaswa kuchukuliwa si zaidi ya saa 48 kabla ya mechi kuchezwa" na taratibu zilifuatwa kama ilivyostahili.

"Na zaidi, baadhi ya wachezaji wa Simba pia walikutwa kuwa na maambukizi pamoja na maofisa [waamuzi] wa CAF."

Barua hiyo ilizidi kueleza kuwa, CAF imefanya uchunguzi kwa kuzingatia taratibu za vipimo vilivyofanyika Tanzania na kubaini kuwa maabara haitoi majibu ama vyeti kwa wale wanaobainika kuwa na COVID-19, na kwamba vyeti hutolewa tu wale ambao hawana maambukizo ya corona na wanaobainika kuwa na maambukizo hutolewa kwa mhusika binafsi ama taasisi husika.

"Kwa hiyo tungependa kuthibitisha kwamba vipimo vya COVID-19 vilivyofanyika na kuwasilishwa CAF ndivyo vilivyochukuliwa kwa kuzingatia mechi kati ya Simba na Al-Merrikh ya Ligi ya Mabingwa Afrika, CL 2020/2021."

Wakati huo huo, jana jioni wachezaji wa Simba waliokuwapo katika kikosi cha timu ya Taifa Stars wameungana na wenzao kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya AS Vita ya DR Congo utakaochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, alisema kikosi hicho kinaendelea vizuri na maandalizi ya mchezo huo na uongozi umewaandika barua CAF ya kuomba kuruhusiwa mashabiki kuingia uwanjani kushuhudia timu hizo zikicheza.

## YANGA SC YAFUNGUKA MUKOKO KAIZER CHIEFS

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imekanusha taarifa zinazosambaa kwa kasi kuwa baada ya msimu kumalizika, kiungo wao mahiri wa ukabaji, Mukoko Tonombe atatimkia Klabu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Ofisa Uhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, amesema taarifa hizo si za kweli na walioandika, kutafsiri, kukosea kwa bahati mbaya au walifanya hivyo makusudi kwa maslahi yao binafsi na kuibua taharuki isiyokuwa ya lazima kwa Wanayanga.

**Habari hizi zilisambaa baada ya klabu ya Yanga kupokea ugeni wa baadhi ya watendaji wa klabu ya Kaizer Chiefs, akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa Tathmini, Usajili wa Wachezaji na Maendeleo ya klabu hiyo, Walter Steenbok na kujionea mambo mbalimbali, ikiwamo jinsi klabu inavyoendeshwa.**

Nugaz alisema, kilichokuwapo ni kwamba mkurugenzi huyo alitaka kujua mbinu za watafuta wachezaji na vipaji wa Yanga walivyowafuatilia na kuwasajili wachezaji Mukoko Tonombe na Tuisila Kisinda nchini DR Congo, wakati wao walichemka.

"Walichosema ni kwamba waliwafuatilia Mukoko na Tuisila wakiwa AS Vita, lakini baadaye walipoenda wakaambiwa kuwa wamechukuliwa na Yanga, hivyo walitaka kujua mbinu Yanga tulitumia kwa sababu hatuna timu ya maskauti yenye uwezo kama wao timu kubwa, lakini wakatupongeza kwa jicho letu kwa wachezaji hao kwa sababu hata wao waliwaona," alisema Nugaz.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002